

KUCHAGUA UPANDE WA YESU



Mahali fulani katika Louisville ambapo una—unakula, na panaitwa... hebu tuone, Hoteli Dogpatch. Nilipata moja leo. Wakati mtu ye yote anapokula pale, ndipo wanachukua pesa ulizowapa na kupelekea kanisa fungu la kumi la hizo. Ni mahali fulani pale 319 Barabara ya Jefferson Magharibi. Nafikiri hiyo ndiyo sababu Billy aliweka hapa, ili waweze kuona. Hilo ni nzuri mno.

² Sasa, wandugu, mimi sijui utaratibu wenu wa—wa mkutano wa manaume, vile mfanyavyo au vile mnaendesha mikutano yenu. Na kama nitatoka nje ya mpango hapa, basi—nje ya utaratibu wa kawaida, basi ninyi nijulisheni hilo.

³ Ilikusudiwa jioni hii, na nikawaza, nilipokuwa nikila chakula cha jioni sio muda mrefu uliopita na mchungaji wetu mpendwa sana, Ndugu Neville, na nilikuwa ninamwambia jambo lililokuwa moyoni mwangu. Na nikawaza ikiwa tutapata kundi la watu pamoja na wahudumu (wao ni wenzetu hapa wa Injili na watu), tungezungumziana kwa njia ambayo hatungeweza kuzungumza hadharani, kwa sababu sote na—tu watu wanaoelewa kama watu, watu Wakristo. Na kwa njia hiyo... Kwa kawaida katika kusanyiko, kundi, unasema jambo fulani, na na mmoja ataliinamisha kidogo upande huu, na mmoja ataliinamisha upande huo, halafu linapotoka kabisa. Lakini tunapokuja kujaribu jioni hii kuwaambia kile nilicho nacho moyoni mwangu sasa, kuhusu kanisa na—mahali pake na nafasi yake. Na tukiwahi kumaliza bila kuchelewa, ningependa kuwahubiria kidogo juu ya Neno, kama ni sawasawa. Ni kama kutuliza hilo tu, ili tupate sehemu ya kazi yetu au ile sehemu ambayo ningependa kuwaelezeni kwanza. Nami nadhani pengine mnafumukana wakati wa kawaida, kama saa tatu na nusu au kitu kama hicho, kila usiku. Vema, nitajaribu nisiwakawishe sana. Kesho ni jumamosi na ni siku kuu ya biashara. Lakini sasa... Yatupasa kupata vyakula vyetu na kadhalika.

⁴ Ningependa kumwambia Ndugu Neville hadharani... Sasa, ningependa kumwambia kila mmoja wenu, kama vile ningezungumza faraghanani nanyi, kila mmoja, kwa sababu mu kundi ambalo—ambalo ni... hakika ninawaza hivyo na kuamini na kufundisha kuwa watu, Mungu amewaweka watu uongozini mwa kanisa Lake, yaani watu Wake. Ona? Na ni... kama nilivyokuwa nikimhubiria Ndugu “Junie” Jackson kule chini jana usiku kuhusu Mungu kuwazingira wa—watu Wake kwa Neno Lake. Na ni mwanamke aliyevunja ile ngome na kupatia fikira nafasi, na ilipofanyika, Mungu daima ameliweka

kwa—kwa mwanadamu alinde Kanisa Lake likizingirwa kwa Neno.

⁵ Sasa, ningependa kumtia moyo Ndugu Neville kidogo tu, nikizungumza naye faraghani. Niliona jana usiku utambuzi ulinjia mara mbili au tatu nilipokuwa mimbarani, kisha nikageuka, kwa sababu ninajaribu kukaa mbali nayo kadiri niwezavyo mpaka nitambue maana yake kwangu ile ndoto ya muda usio mrefu uliopita, majuma kadha yaliyopita. Ilikaa nami kwa muda mrefu; nilieleza hapa kanisani, kuhusu—jambo fulani kuhusu Ujumbe na—na utambuzi na kadhalika; haikuwezekana—haikuwa inajitokeza sawasawa. Kwa maoni yangu, wakati huo umekwisha, na sasa huenda nimekosea juu ya hilo, lakini niliona kuwa—kuwa Ndugu Neville alikuwa kama mchovu na anahangaika.

⁶ Na ndipo nikataka tu ujue, Ndugu Neville, kwamba wewe unatumainia tu katika ushirika huu katika jambo hilo. Je mmeona yale ambayo Shetani amejaribu kufanya katika siku chache zilizopita kwa wahudumu wanaoshiriki katika ushirika huu? Tulieni kwa dakika chache na kuwaza. Hapa Ndugu Crase ameketi, akikaa hapa usiku huu, karibu auawe pale barabarani. Ona? Na mimi karibu kulipuliwa kichwa changu na bastola—au na bunduki. Ona? Shetani akijaribu kutuua. Na pale ukapata ajili na ungejiva pamoja na mwanamke fulani pia. Ona, ni wahudumu tu. Tazama tu lile—lile kundi la wahudumu. Ona? Ni Shetani, na anajaribu kutuungamiza.

⁷ Sasa, tuna—tunatambua kwamba hatukukusanyika hapa kuongea juu ya biashara fulani; tuko hapa tukutane tuzungumze juu ya ile—juu ya Kristo na vizuizi vinate, na la kufanya kwa wakati huu uliopo. Na ni—ninataka kukutia moyo, Ndugu Neville. Uwe na ushujaa. Hata itoke nini, iende nini, itendeke nini, usiruhusu lo lote likukwaze. Simama tu pale kama mwamba wenye imara na Mungu atafanya yote yatendeke sawasawa; ameyathibitisha hayo kwako. Bila shaka, hiyo ingekuhangaisha; hiyo ingemuua yule mwanamke, ni hilo lingekaa fikirani mwako siku zako zote zilizosalia, na yangukuwa mambo mengi. Lakini Mungu angali kwenye Kiti cha Enzi; Yeye—Yeye huruhusu hayo yatendeke sawasawa. Angetuchukua pia. Na . . . Basi, Shetani akipigana na Kanisa.

⁸ Sasa nilipoliweka lile jiwe la msingi asubuhi hiyo, sikujisikia kwamba ningekuwa mchungaji wakati wo wote. Halikuwa katika mwito wangu mwanzoni, na mwito wangu wa kwanza ulikuwa kuwa katika ule uwanga wa uinjilisti. Hiyo ni miaka mingi iliyopita, na ilianza pale ng'ambo katika hema, ng'ambo ya hii barabara. Na ninakumbuka wakati ambapo Ndugu Roy Davis, pale chini, na kanisa lake likateketea. Kundi hilo la watu lilikuwa kama kondoo waliotawanyika bila mchungaji; hawakuwa na mahali pa kuenda. Na mimi . . . Bwana Hibstenberg alikuwa Mkuu wa Polisi wakati huo, na akaniita

kule chini na kuniambia, “Tuko hapa kuwasaidia ninyi.” Kasema, “Mimi mwenyewe ni Mkatoliki, lakini” kasema, “hao watu,” kasema “hawana... pengine hawana nguo.” (Ilikuwa wakati wa kule kushuka kwa uchumi.) Kasema, “Wanaenda kwa makanisa mengine na kujisikia kama waliopotea, na ni watu wazuri. Na ninawajua wengi wao.” Akasema, “Billy, ikiwa unataka kuanzisha kanisa,” akasema, “ningetaka ujue kwamba tuko nyuma yako katika lo lote tunaloweza kufanya kukusaidia.” Na nilimshukuru kwa hilo.

⁹ Tulikuwa na siku ya vibandiko. Kwanza tuliomba na kumsihi Bwana, na watu wakanijia na walitaka kujenga kanisa ili wapate kuwa na mahali pa kuenda. Na tukaamua mahali hapa, na usiku moja yapata wakati huu (au mbali na hapa kidogo) katika fungu dogo la magugu papa hapa ndani na maji katika mtaro huu na palikuwa tu kama mahali pa kutupia takataka, vema, Bwana alinizungumzia dhahiri na kusema, “Lijinge papa hapa.” Hamna hata ndururu—na sote pamoja tulikuwa na karibu senti themanini au dola moja. Na hiyo ni... Ndiyo, mnaweza kucheka kusikia hayo sasa, lakini Ndugu, hiyo ilikuwa pesa siku zile!

¹⁰ Wakati jirani fulani angepika nyungu ya maharagwe na amuite jirani yake ambaye hakuwa na cho chote kwa siku tatu au nne aje kwake na kula kidogo, hizo zilikuwa nyakati ngumu. Vijana wengi hawajaona hayo, lakini huo ulikuwa wakati mgumu. Nimeona wakati ambapo ungepitisha sahani ya sadaka, mara mbili au tatu, na kupata senti thelathini kutoka kwa mahali palipo jaa kabisa, na baada ya kuwaomba watu. Ingekuwa... Pengine ungepata senti thelathini na hiyo iwe ni sadaka nzuri. Ona? Ni wakati wa taabu sana.

¹¹ Na hatukuwa na cha kujengea, hata hivyo ile—shauku ya watu ilikuwa kujenga kanisa ili tuwe na mahali pa kuenda, kwa sababu katika siku zile Ujumbe... Naam, mwadhani unafikiriwa mabaya sasa, laiti mngaliujua siku zile, ambapo hapana mtu. Na ndipo—huu ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo na hizi baraka na mambo tunayoamini na kuyazingatia.

¹² Kwa hivyo moyoni mwangu nikamuahidi Mungu kwamba tutakaa hapa na kuyajenga maskani. Asubuhi ile tulipoweka jiwe la pembeni, Yeye alikutana nami pale katika njozi yapata saa mbili asubuhi ile, nilipokuwa nimeketi pale nikitazama kule ng'ambo jua likichomoza, yapata wakati kama huu wa mwaka. Na Yeye aliisha niambia, baada ya Yeye kukutana nami pale chini mtoni, lakini ile... Wakati yule Malaika wa Bwana alipoonekana katika ile Nuru, na mimi nikaiona ikiwa mbali, ilionekana kama nyota, na ikashuka moja kwa moja mpaka nilipokuwa, na hayo maneno muhimu yakasemwa. Na ndipo basi, nikanuia wakati huo kupata mahali pa watu kuabudia.

¹³ Sasa, nikafikiria mwenyewe, “Si Langu. Si kitu kwangu, lakini hata hivyo cho chote kinachomhusu Mungu ni sehemu yangu, si hoja kama ni. . . Cho chote ambacho—ambacho ni cha watoto wa Mungu, ni changu, iwe ni wajibu wangu kufanya hili au kufanya lile. Ni wajibu wangu kuangalia hili au kufanya lile. Ni wajibu wangu kuangalia warithi wa Mungu bila kujali mahali walipo.” Ona?

¹⁴ Ni kama tu vile ungalisema, “Vema, kazi. . .” Kama ungalikuwa mvulana mdogo, useme, “Ka—kazi yangu ni kukata kuni tu, si kuziingiza ndani. Yohana na aziingize ndani. Sijali hata kama barafu ingalizimwagikia, mvua; hebu atoke akazichukue? La, ni kazi yako kama m—mtoto wa nyumba hiyo kuona kwamba kuni hizo hazilowi maji kwa ajili ya mama yako. Ona? Ziingize ndani.

¹⁵ Ikiwa wanasema, “Naam, Frank alipaswa aende alete maji; hiyo si kazi yangu.” Lakini kama Frank hakuenda kuleta maji, ni kazi yako kuangalia habari ya maji. Hivyo tu. Sasa, hivyo tu ndivyo inavyotendeka, na hivyo ndivyo inavyotendeka katika jamaa ya Mungu pia.

¹⁶ Kama baadhi yao. . . Baadhi yao walisema mwingine—sio muda mrefu uliopita, walisema, “Acha kuhubiri vile unavyofanya. Ole wangu, utamharibu kila rafiki uliye naye na mambo kama hayo.” Wakasema, “Liache hilo peke yake; najua ni kosa, lakini wee, sio kazi yetu.” Naam, ni kazi ya nani basi? Ikiwa ni kosa, mtu fulani lazima alifanye. Basi hebu natulifanye tu. Na hivyo ndivyo ninavyoona kuhusu kanisa.

¹⁷ Ile mipango ya ujenzi na mengineyo imekuja juu chini, juu chini, na kumekuwa na kupendelea na kupinga ujenzi na kadhalika. Mmoja alitaka na mwingine hakutaka na hili, lile. U—unalikuta hivyo.

¹⁸ Unakuta hayo unaposhughulika miongoni mwa wahudumu, miongoni mwa wafanya biashara, miongoni mwa vyumba vya kupanga—po pote uendapo ambako kuna kundi la watu, u—una maoni tofauti. Na kwa hivyo basi, lazima muwe na mtu mmoja mnayemtumaini, na kumchagua mtu huyo, na wote wanafanya kazi naye. Kama tu katika jeshi, lazima uwe na. . . Mmoja ni jemadari; hayo ni makao makuu. Kapiteni asema hivi; yeye ni kapiteni wa kundi hilo, lakini jemadari anaweza kugeuza amri zake. Na Jemadari Mkuu Anayeamrisha, bila shaka, ni Yesu Kristo katika Kanisa na wahudumu Wake ndiyo makapiteni wake wa makundi wanoa—wanaomuakilisha Yeye hapa duniani.

¹⁹ Na wamejaribu mambo mengi, haya maskani madogo hapa, na hatimaye. . . Nilinyamaza katika hilo, ili kuona tu, baada ya kuyajenga. . . Na ndipo Bwana akaniita nje uwanjani yapata miaka kumi na mitano, kumi na sita iliyopita, na nikaliacha kanisa. Lakini hata hivyo, siwezi kuliacha. Nimelihusisha jina langu kwayo kila mara, kusudi nipate kupiga kura kama

jambo lo lote baya lingezushwa hapa; ningekuwa na haki kuja na—na kulikomesha, kwa sababu daima nimetoa jasho miaka mingi nyuma ya mimbara hii—miaka kumi na saba kunyosha jambo hilo. Wakati kila namna ya *mafundisho* na *ndani* na *nje* na kila namna ya makundi yaliyojitenga... Huku tukiwa hatubagui dini, kila kitu kilichoruka ndani, kililingia hivi, na kwa msaada wa Mungu tulisimama hapa na Injili isiyogoshiwa, na yangali yaumesimama vivyo hivyo usiku wa leo. Na kwa hivyo sisi... Bali... Kuna wakati ambapo kanisa hili limejaribiwa kuuzwa chini yangu na mambo kama hayo. Kama jina langu halikuhusishwa nalo kule chini, naam, bila shaka lingekuwa—lingekuwa katika matatizo mabaya sana usiku wa leo, si... Na haikuwa mimi, ilikuwa Mungu, bila shaka, ambaye alifanya hivyo.

²⁰ Halafu, ninavyoliona sasa, limefikia mahali lilipo, nasi tunaishi katika wakati wa ajabu, ingali ni mapenzi yangu kusema jambo fulani kuhusu kanisa hili. Ona? Kwa sababu ni—ni sehemu yangu. Si hoja kama niko hapa ama siko, lingali sehemu yangu. Na ni jukumu langu kuona ya kwamba linatenda kazi vizuri, dhahiri, na vyema sana niwezavyo kwa Utukufu wa Mungu. Nami nashukuru ya kwamba katika siku hizi...

²¹ Naona kwamba lina mengine mashirika yake ambayo ninafurahia. Ndugu Crase hapa na kikundi chake cha Sellersburg, na yule ndugu kule nyuma ambaye ndiyo kwanza apachukue mahali pa Ndugu Snelling kule Utica, na Ndugu Ruddle juu hapa, na Ndugu Junior Jackson na hao vijana wapendwa ambao ni watu wazuri, watu wa ajabu wa Mungu; wao wanahubiri Ujumbe huu. Sasa, wao walifanya... Mmoja anaweza kutokukubaliana kidogo juu ya jambo moja ama lingine; huo bado ni ubinadamu tu kati ya kundi la wahudumu. Na iwapo wahudumu wana tofautiana kidogo... Hapatukuwepo na—na uvuli wa kutofautiana kwake. Huenda mmoja akasema, “Naamini ule Utawala wa Miaka Elf utakuja naye Yesu atakuwa juu ya farasi mweupe,” na mwingine aseme, “Naamini atakapokuja Yeye atakuja juu ya wingu jeupe.” Vema, mradi tu wanaamini Yeye yuaja hilo ndilo jambo muhimu. Haidhuru atakuja vipi hebuni tu... aminini ya kwamba Yeye yuaja na mwe mkijitayarisha kwa ajili yake. Na kwa njia hiyo...

²² Nimejaribu kuona sasa, nami nimekuwa nikisoma (sasa nimekwisha kulisema mbele ya waumini), nimekuwa nikisoma kirefu lile Kanisa la mwanzoni, nami nimeona jinsi hao watu waliotiwa mafuta waliitayarisha Nyumba ya Bwana na taratibu ya ibada ya Bwana katika Nyumba ile, nalo likanigusa sana—likanifariji sana. Nami nimehubiri hapa wakati mfupi uliopita na—juu ya somo la Yoeli 2, “Nitarudisha, asema Bwana, hiyo miaka yote iliyoliwa na tunutu, na madumadu, na parare na kadhalika.” Nami nikaanza kusoma hayo, jinsi hawa watu

walivyofanya, na jinsi walivyolishughulikia Kanisa ambalo Mungu aliwaachia kuwa waangalizi.

²³ Sasa, tutaanza na lile Kanisa la mwanzoni na kulileta tu (kwa yapata dakika tano sasa) kufikia kwa yale waliyofanya, kisha naweza kuwaonyesheni ono nililo nalo kwa ajili ya siku za usoni. Sasa, hapo mwanzo, Kanisa liliadhimishwa katika Pentekoste. Na hapo Roho Mtakatifu akawashukia ambapo Yesu alikuwa amewachagua kumi na wawili. Na mmoja wao aliisha kuanguka, nao walikuwa wamemchagua Mathiya kupachukua mahali pake, naye Roho Mtakatifu alingoja hata hayo yote yalishawekwa katika taratibu kabla hajaja. Iliwabidi kumchagua mtu mmoja kupachukua mahali pa—pa Yuda, aliyeanguka kwa maasi kuyatimiza Maandiko.

²⁴ Nami naamini ya kwamba mambo haya yote yana wakati wa kudumu, kwa siku nyingi, kungoja; lakini ni kungoja wakati Maandiko yatakapotimizwa, hata kila kitu kitakapokuwa sawa, kila kitu katika taratibu, vikingoja. Wakati mwingine tunapata subira—kukosa subira. Kama mtoto mdogo, tunapata—tunatazamia sana ya mbele sana na mara nyingi tunaruka mbele sana, na hilo—hilo huzuia tu kazi, hata kazi inacheleweshwa. Ona? Inatupasa kuenenda tu kwa hicho, kuwa na kusudi moyoni kwamba Mungu, iwapo angetaka kututumia kwa njia *fulani na fulani* . . . bali subiri hata Yeye atakapofungua njia, maana hana budi kwenda mbele zetu.

²⁵ Mnakumbuka Daudi alipokuwa akienda vitani usiku huo? Alikuwa ameisha kuchoshwa na vita hivyo, naye akalala chini ya miforsadi hata alipomsikia Bwana katika mingurumo ya majani akienda mbele yake; ndipo yeye akaondoka akaenda kwa ushujaa, kwa sababu alijua ya kwamba Mungu aliisha kwenda mbele zake. Laiti tungalifanya hivyo, ndugu zanguni, tukijua ya kwamba vita havina budi kuja; bali hatuna budi kungoja hata tutakapouona mkono wa Mungu ukienda mbele zetu kututengenezea njia.

²⁶ Basi, naona jinsi makanisa, uinjilisti ulianza kusambaswa kila mahali. Kisha tutachukua, kwa mfano, yule—Paulo akiwa mmishenari mashuhuri kwa watu wetu. Tunaona ya kwamba yeye alienda kila Bwana alikomtuma, naye akaanzisha kanisa. Nayo ilikuwa imani mpya. Makanisa ya siku hizo, kama katika Asia Ndogo, kote katika Uropa, wao—wao hawakuamini Ujumbe huo. Na alipokwisha kuuhubiri Ujumbe huo, na wengi wakaongoka Kwake, basi hakukuweko mtu ye yote. . . Kama aliwaacha watu katika hali hiyo, wao wangelirudia miungu yao ya kishenzi, na kuingia Uyuda, na kadhalika, kwa kuwa watu hao hawakuwa na ye yote wa kuwafundisha wale—wale waongofu. Hawakuwa na pa kwenda, kwa hivyo Paulo akaanzisha makanisa mahali mbalimbali nchini.

²⁷ Kila moja ya makanisa haya, aliacha mtu mmoja aliyefaa, mtu mwaminifu, mtu aliyejulikana kama mchungaji, ama... Kisha baada ya kanisa hili basi, yakazuka... Makanisa mengine madogo yakatoka kwake. Vijana kwa wazee wakainuka wakawa makanisa kutoka kwa hilo. Mtu aliyeliongoza kanisa la kwanza aliitwa askofu. Ndiposa wale, hao waliotoka kwake, watoto wake, waliitwa wachungaji wa kondoo au wachungaji. Halafu kundi hili la makanisa madogo madogo yote yangerudi kwa askofu huyu.

²⁸ Kama katika wakati wa Irenaeus, yeye aliendeleza jambo lile lile. Martin aliendeleza jambo lile lile. Polycarp aliendeleza jambo lile lile. Kote kote katika zile nyakati walikuwa na hayo. Ndiposa yule mtume wa kanisa, aliyekuwa—Paulo... Na Paulo alipoondoka, Yohana akashika uongozi juu ya kanisa. Kisha Yohana alipoondoka Polycarp akachukua uongozi. Polycarp alipoondoka, Irenaeus akachukua uongozi, na kwendelea, na Martin na—na kadhalika. Ikazidi kuendelea hata Kanisa Katoliki la Rumi lilipovunjilia jambo hilo lote kabisa na kuwachoma moto na kuwatawanya; na tunutu akala *hili*, na parare *kile*, hata walipolifikisha hata kwenye ubua.

²⁹ Naam, bali Mungu aliahidi kurudisha tena kitu hicho hicho. Nina—ninaamini kwa moyo wangu wote ya kwamba tuko katika siku za mwisho. Naamini ya kwamba hakuna wengi sana wangelibishania hili...cho chote... (na huenda ikawa fasiri yangu ya Maandiko si kweli) ya kwamba Yesu hangalikuja usiku wa leo. Naamini hivyo—yale machache yaliyosalia kutimizwa yangelitimizwa kabla ya kupambazuka asubuhi; nami naona—na huenda nikakosea katika wakati wa kutimizwa huko, bali kumekaribia. Hayo...naamini hayo. Na kumbukeni. Paulo aliamini hayo; Yohana aliamini hayo; Polycarp aliamini hayo; Irenaeus aliamini hayo; Martin aliamini hayo; wote wengine waliamini.

³⁰ Vipi kama Mungu angalimwambia Yohana Mfanusi, “Itakuwa miaka elfu mbili kabla ya kuja Kwangu?” Yohana angalirudi na kuliambia Kanisa, “Vema, nakisia afadhali tule, tunywe, na tufurahi, kwa maana kutakuweko na vizazi vingi. (Ona?) Yesu hatakuja hata itimie miaka elfu mbili.” Ona? Kwa hivyo...Ona, Kanisa liisha kuwa legevu; hakungelikuwa “iweni tayari”; hakungalikuwa na kukesha. Hata hivyo ni, ni yale matumaini yako. Ukilala katika sehemu hiyo ya kukesha utaamka na mtanzo uo huo, kwa kuwa haitakuzuia kwa jambo lo lote, utakuweko kule kwa wakati haidhuru. Ona? Mnaona ninayomaanisha?

³¹ Sasa, wa—wakati Mt. Martin atakapoamka katika ufufuo, Mt. Paulo, wengine wote, itakuwa jipya tu kana kwamba wao walikuwa moja kwa moja vitani, wakipigana vikali, kwa sababu walienda moja kwa moja chini ya matumaini hayo, wakitazamia

kuja Kwake. Na kutatokea mlio, na Kanisa lote litafufuka. Mnaona? Hiyo itakuwa ndiyo. Kwa hivyo haijalishi.

³² Ona, inatupasa kuwa tukimtaamia sasa hivi. Hata... Hatujui. Huenda—huenda ikawa... huenda ikawa miaka mia moja tangu sasa, huenda ikawa miaka mia tano, miaka elfu. Sijui. Hamna anayejua. Bali tuseme kwa mfano, kwamba tuishi kila siku kana kwamba alikuwa yuaja siku hiyo. Ona? Kama tukiishi kana kwamba alikuwa yuaja siku hiyo, tutakapofufuka (kama tukilala na kufufuka katika ufufuo), itakuwa jipya tu kana kwamba ndiyo kwanza tumelala usingizi, ndiyo kwanza tuamke. Parapanda italia nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza; sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani. Ona? Kwa hivyo itakuwa jipya tu.

³³ Lakini sasa, hata wakati huo, hata atakapokuja, tunataka kuishi kila siku kana kwamba huenda akaja dakika ijayo, kwa kuwa huenda ikawa mwisho wa uhai wako dakika hiyo. Haujui utaondoka lini. Hii huenda ikawa baadhi ya pumzi zetu za mwisho; tunazo ndani yetu sasa, kwa hivyo unataka kuishi kama kwamba ndiyo ilivyo.

³⁴ Lakini sasa, kupiga hatua nyingine, inatupasa kuweka nyayo zetu hapa kwenye changarawe za wakati kusudi wengine wapate kuona. Paulo asingaliendelea jinsi alivyoendelea, basi Yohana hangalijua jinsi ya kufuatilia. Yohana asingaliendelea mbele, Polycarp hangalijua jinsi ya kufuatilia. Polycarp asingaliendelea, Irenaeus hangalijua jinsi ya kufuatilia. Irenaeus asingaliendelea mbele, Martin hangalijua jinsi ya kufuatilia. Mnaona ninayomaanisha? Kila mmoja hana kuweka nyayo kwenye changarawe za wakati.

³⁵ Vema, kama ningaliwazia ya kwamba kulikuweco dhehebu ama kundi lingine lo lote la waamini waliokuwa na cho chote bora kuliko tulicho nacho hapa, ndugu zanguni, ningalitaka kuunganisha kundi hili ndogo nalo upesi sana. Nimengoja, nimekuwa na hamu, nimekuwa na matumaini na kuamini ya kwamba mtu fulani mkuu yuaja siku moja ama huenda ikawa na—nabii mkuu ninayenena habari zake yuaja, wa yule Elisha. Daima nimeamini na kuwazia ya kwamba labda nitaishi kuiona siku hiyo, wakati ningebadilika, wakati nitakapomwona mtu huyo ameinuka jukwaani. Ndiposa ningechukua kanisa langu ndogo na kusema, “Ndugu zanguni, huyu ndiye yule mtu tumekuwa tukimngoja. Mtu huyu, ndiye.” Nimengoja hilo. Na iwapo hiyo imetendeka basi ninatarajia kusema kutoka hapa juu “Ndugu zanguni, huyu Ndiye.” Akija kutoka *hapa*. Ona? Nami ni—ninataka kanisa liwekwe hivyo.

³⁶ Hapana budi nimekanyaga kitu fulani ama kufanya jambo fulani na kukifanya kitu hicho kutoa sauti nyi—nyingi. [Ndugu

Branham amekanyanga waya za maikrofoni zikatatiza uenezaji wa sauti.—Mh.]

³⁷ Kwa hivyo sasa, ningetaka kusema haya. Ya kwamba kwa kuwa hili ni kanisa lililoimarishwa. . .

³⁸ Hebu nikome tena kidogo. Nilipoenda kule Bombay. . . (Nahesabu huo kuwa mkutano wangu ulio mkuu sana kwa sababu ya matokeo yake kwa watu.) Nami. . . Kama katika Africa, wao wanasema elfu thelathini walimjia Kristo wakati mmoja, kisha kulikuweco na elfu mia moja na hamsini ama elfu mia mbili waliomjia Kristo Wakati mmoja kutoka kwa hao nusu milioni kule. Ningefanyaje? Hapakuwepo kitu. Labda, tuseme kulikuwa—tuseme kulikuweco na watu elfu mia moja. Hapakuwepo na kanisa lo lote, singefanya kitu. Hapakuwepo na mtu ambaye ningelimkabidhi hao. Ujumbe nilioamini, hamna hata dhehebu la Kipentekoste lingalishirikiana nami. Na watu hao wote labda walirudi kwenye Washiites, Wajains, Ubuddha na ko kote walikotoka. Hamna mahali pa kuwaweka. Sasa, hiyo ni aibu; hiyo ni fedheha (ona?), kwa sababu sikupata ushirikiano, kwa sababu ya msimamo ninaochukua. Ona?

³⁹ Vema, katika Afrika, nilienda kule kwa msaada wa A. F. of M. na (Afrikaans Faith Missions)—na nilipofanya hivyo. . . Hakika, siwezi kukubaliana nao. Wao—wao huwabatiza watu chini ya ubatizo wa utatu, mara tatu uso mbele; na moja yao hubatiza mara tatu nyuma: moja kwa Mungu Baba; ya pili kwa Mungu mwingine, Mwana; halafu kwa Mungu mwingine, Roho Mtakatifu; na kubatiza mara tatu mbalimbali kwa miungu mitatu mbalimbali na upuzi kama huo. Na labda ule mkutano wa Durban, kwa kutoipata sawa—na watu wanaona kutengana kwingi sana kati ya madhehebu ya Kipentekoste na kadhalika, watu hawakujua wafanyeje. Ha40kuwa na mahali pa kwenda.

⁴⁰ Labda, vipi kama tungalikuwa na ufufuo hapa, ndugu zangu. . . Hebu niliweke hivi. Vipi kama ndiyo kwanza tumalize ufufuo mkubwa nanyi ndugu ndiyo kwanza muongoke, na hapakuwepo na kanisa la namna hii mahali po pote nchini; nami nilikuwa mwinjilisti, na sasa naondoka na hamtaniona tena? Mngelifanyaje? Mngelijisikia kama. . . Hamngalijua la kufanya. Hamngalirudi kwenye hilo boma tena. Hamngalirudi kule chini pamoja na—na wake zenu wakavalie surali fupi na—na karamu zenu za kadi, na mambo kama hayo, na mpate kushiba tena. Mmekuja kwenye Nuru; mmeinuka juu ya kitu hicho. Mmefikia mahali badala ya kusema, “Hii ndiyo kanuni yetu ya imani.” mnasema, “Hili ni Neno la Mungu.” Nanyi mmeanza kuishi kwa *Hili*, yale *Hili* lisemayo, na si yale. . . Na mwende kule chini na kuwasikiza, na kuwasikia wakishuka kwenda na kucheza michezo, na kucheza dansi, na *hivi*, *vile*, na *vinginevyo*, na ujumbe mdogo ambao hamna kitu ndani yake (juu ya meya fulani na kadhalika ambaye atachanguliwa tena, ama namna fulani ya mambo ya kisiasa), na kuumaliza katika muda wa

dakika kumi ama kumi na tano; baada ya ninyi kuketi hapa siku baada ya siku na sikukuu ya mlo mkubwa wa Neno na kadhalika, hamngalijua la kufanya! Mngalilemewa sana nayo, hata baadhi yenu waumini mngejisikia kama mnganzisha kanisa na kuanza kuhubiri humo, kwa maana mioyo yenu ingaliwaka moto kwa ajili ya Neno la Mungu, nanyi mangesikia vibaya kwa ajili ya watu waliosikia vile vile kama ninyi mlivyosikia. Naam, siyo?

⁴¹ Ingawa unajua Yesu yuaja, ingawa yuaja kesho, hata hivyo ungetaka kufanya jambo fulani leo kwa ajili ya watu ambao ni raiya pamoja nasi wa Ufalme wa Mungu, kukutanika pamoja; ungalitaka ushirika pamoja nao. Hiyo ni kweli. Kwa hivyo, ikiwa ndivyo ilivyo. . .

⁴² Sasa, naamini kwa moyo wangu wote ya kwamba Bwana amenisaidia na amenitumia kuazilisha ufufuo mkubwa, mmoja wa iliyo mikuu sana iliyopata kugusa ulimwengu tangu siku za mwanzoni—kote ulimwenguni. Tunajua hivyo. Hiyo ni kweli. Ilikuwa yote imekwisha wakati huo, na—naye akanijia kule chini na kule mtoni na kuniambia ya kuamba Ujumbe niliokuwa nao ungetangulia kule kuja kwa pili kwa Kristo. Nami nadhani hamna mtu hapa usiku wa leo aliyekuwa kule chini wakati huo. Hiyo imekuwa miaka thelathini na miwili iliyopita, wakati hiyo Nuru ilipoonekana, nami nimesimama pale, nikiiangalia, na mamia ya watu wamesimama wakiiangalia, Ilishuka moja kwa moja chini na hiyo Sauti ikanena.

⁴³ Miaka mingi baadaye—ni ajabu kwamba kamera ilichukua picha ile ile, inafanana na kitu kile kile, jinsi hasa nilivyowaambieni, kule chini mtoni. Sasa, huenda nikakosea katika mambo mengi, ndugu zanguni, lakini sitaki kuwa mnafiki. Nataka kuwa mwaminifu na mnyofu kwenu.

⁴⁴ Halafu, jambo jingine, kama ningaliondoka, vipi—hatungalijenga kanisa hapa kama hilo. Ni vigumu kusema tungalikuwa na nini (ona?) kama ningaliendelea tu, lakini Mungu wa Mbinguni akanihimiza moyoni mwangu kujenga kanisa hili hapa. Ndiposa aliponiita kuingia katika ujilisti. . . Tumekuwa na mchungaji baada ya mchungaji na kadhalika, lakini sasa tuna ndugu mpendwa hapa ambaye ni wa imani hii, anaamini Ujumbe. Tuna ndugu wengine humu wanaoamini Ujumbe, wakiwa na mambo. . .

⁴⁵ (Ninasema kwa sauti kubwa sana, Ndugu Beeler?) [Ndugu Branham anazungumza na Ndugu Beeler—Mh.] Tulikuwa—tuna—tuna vifaa.

⁴⁶ Na sasa, mnasema, “Vema, Ndugu Branham, iwapo hawatasikia ishara hizi na maajabu ya Mungu mkuu wa Mbinguni, tutafanyaje?” Vema, sasa, vipi kama Mt. Paulo alikuwa na wazo lilo hilo? Ona? Vipi. . . Bali hakuwa nalo. Hao maaskofu walidumu waaminifu tu kwa Ujumbe, nao—na Paulo mara kwa mara, baada ya kuzunguka kwake. . . Mmeisoma

Biblia, jinsi angeyatembelea tena haya makanisa, azungumze na wachungaji pamoja na maaskofu na kadhalika, na kutoa faraja kwa watu na—naye alikuwa na—lo, wakati mkuu wa ushirika, kama ufufuo ama wakati mkuu wa sikukuu; na Roho Mtakatifu angeshuka juu yao na jumbe zingekuja.

⁴⁷ Tazama aliposhuka kwenda kule kwa Filipo, hata binti zake walitabiri wakisema, “Minyororo na vifungo vinamngoja ndugu yetu atakapofika kule.” Mara tu alipofika uwanjani huyu hapa Agabu akija, nabii, akija, akatazama upande wa pili wa barabara, na hakuwa amepata kumwona Paulo hapo awali, yule mwangalizi mkuu wa kundi hili lote la makanisa katika Asia nzima. Naye akaenda kule na kuutoa mshipi kiunoni mwake uliokuwa umelifunga vazi lake, akaifunga mikono yake akasema, “BWANA ASEMA HIVI: minyororo na vifungo vinamngoja yule aliyevaa huu kule.” Ona, akitoa unabii.

⁴⁸ Paulo alisema, “Najua hivyo; najua hivyo, lakini usije ukauvunja moyo wangu sasa. Hebu nimalize mwendo wangu.” Yeye alikuwa amechoka; alikuwa amekwisha; naye alikuwa anaondoka na kumwachia Timotheo mahali pake.

⁴⁹ Sasa, inatubidi kuwaza habari za vijana. Tuna watoto. Wengi wetu watu hapa, watu waliooa, wana watoto. Je, na wale wanaokuja je? Ona?

⁵⁰ Kama nilivyokuwa nikiwapinga wao kuhusu kutupa hizo nyavu mtoni na kuwavua samaki wa maji matamu na wanywaji—walevi na kadhalika... Nimewaona wamerundikwa juu kwa juu hata kwenye dari hii hapa, samaki wakubwa na wazuri wamewekwa pale; mnuko ungekuwa kote mtoni. Nilishuka nikaenda kule kama mlizi wa wanyama wa pori kuwafanya wakomeshe hayo. Nikapata barua: “Waache.” Utafanyaje, ni wa Kentucky. Sasa mlinzi wa Kentucky hawezi kuja hapa, kwa sababu ametoka nchini mwake. Mlinzi wa Indiana hawezi kusema neno, kwa sababu maji hayo ni ya Kentucky. Naam, hamna la kufanya.

⁵¹ Nilisema, “Nina mtoto anayekua ambaye angetaka kuvua samaki. Naam, wangelibandika picha yake gazetini kama angalivua samaki mdogo miaka ishirini tangu sasa, hebu hayo yaendeleo hivyo—hizo nyavu, mitego na kadhalika.” Na sasa inakuwa hivyo sasa hivi. Ona? Ni nini? Hamna budi kuwafikiria hawa wanaokuja.

⁵² Kwa hivyo hatuna budi kuwafikiria wengine wanaokuja nyuma yetu, vijana hawa na kadhalika, na mahali kwa ajili ya watoto wetu. Binti zetu, hatuwataki kule nje ulimwenguni katika mambo haya hivyo; tunawataka hao wasichana wapate malezi kama ya mama zao. Na inatupasa kufanya mipango hiyo. Na iwapo hamna kesho, hatujui hivyo. Iwapo hamna ya kesho, hatujafanya jambo lo lote na tumekutwa mahali panapotupasa ajapo. Ona?

⁵³ Kwa hivyo ningeshauri hivi; nilifanya hivyo kwa Ndugu Neville. Hebu tuendeleze hili jinsi tumefanya. Hebu tuliache tu jinsi lilivyo. Ninashukuru kwa ajili ya wahudumu hawa vijana. Ona, kweli kwenye Siku ya Hukumu, bonde hili lote kupitia hapa halitakuwa na udhuru, kwa sababu tuna makanisa madogo yaliyo kila mahali—minara, minara ya kusikizia, yakingoja.

⁵⁴ Usiku uliopita nilikuwa katika kanisa la ndugu fulani na nikauliza iwapo hao wote walikuwa wamekingwa na Neno, na kila mkono ukainuliwa. Sasa, hilo lilinifanya nijisikie vizuri. Ona?

⁵⁵ Sasa, yale ningewazia yangekuwa haya, ndugu zanguni, ya kwamba kama katika kanisa hili hapa, sasa, mimi—ile—huduma yangu ina, nijuavyo mimi, mambo manne ambayo yanaweza kufanywa; na huenda yasiwe yote manne, bali huo ndio mtazamo ninaoweza kuwazia. Kama Huyo aliyenena nami kule chini mtoni. . . Kama haya ndiyo yote yaliyosalia kwa ajili ya kanisa la Mataifa—ambapo katika Ufunuo inasema sura moja, mbili, tatu kwa ajili ya Kanisa. Kanisa linanyakuliwa katika sura ya 4: halirudi tena hata sura ya 19—hiyo ni baada ya wakati wa ile dhiki Mungu atakapowaita Wayahudi. Hiyo ni kweli.

⁵⁶ Na kama Henoko, yeye alinyakuliwa kabla tone moja la mvua halijagusa dunia. Aliondoka; kisha ile dhiki ikaanza. Ona? Nuhu alikuwa safinani kabla dhiki yo yote haijaanza. Lutu alikwisha kutoka Sodoma kabla dhiki yo yote haijaanza. Ona? Na kanisa litaondoka kabla ya wakati wo wote wa dhiki.

⁵⁷ Sasa, katika dhiki itakayokuja, yule mwanamwali aliyelala atawindwa na lile joka (atatupa maji kutoka kinywa chake, ambayo maana yake ni makutano na watu, majeshi) ambao watamtafuta na kumchukua mwanamke huyu, wazao wake waliosalia, nao watamuua. Sasa, hiyo itakuwa katika ule wakati wa ile dhiki, lakini kanisa litaenda nyumbani. Sasa, kama—kama hiyo itachukua—itatendeka kesho, haingetuzuia kuendelea leo. Hebu na tufanye leo iwe na maana.

⁵⁸ Sasa, ninayowazia kule chini, kama yule Malaika aliyeniambia maneno hayo, kasema, “Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kule kuja kwa kwanza kwa Kristo (ona?), Ujumbe wako. . .” Ilikuwa nichukue Ujumbe huu nao ungetangulia kule kuja kwa pili kwa Kristo. Vema, kama huu umekuwa ndio, basi tumekaribia sana, sana, ndugu zanguni, kwa sababu ile saa na ile Nuru ya Ujumbe imekaribia kwisha.

⁵⁹ Je, uliona wakati Pentekoste ilishuka na hao ndugu wakajazwa kule Pentekoste na Roho Mtakatifu, haikuchukua wakati wo wote hata Ujumbe ulipoanza kudidimia nao wakaanza kuanzisha makanisa kushikilia ngome kwa ajili ya Kristo, wakimtarajia Yeye aje. Vema hilo ndilo jambo lile lile linalotendeka leo. Kama Maandiko ni kweli, “Nitarudisha, asema Bwana, yote iliyoliwa na tunutu na parare,” sasa, kama

hiyo ndiyo, kama huo ndio Ujumbe (na Mungu anisamehe, si—sijui), kama huo ndio, basi wakati umekaribia kwisha, kweli, kwa sababu Ujumbe umekwisha.

⁶⁰ Na usiku uliopita niliota ya kwamba nilienda kufanya utambuzi mahali ambapo kundi kubwa la marafiki zangu walikuwa wamekusanyika—maelfu yao—mkutanoni. Mtu fulani alikuja akanipata na... (Billy Paul huja kunichukua, maana hazungumzi nami.) Na mtu huyu alizungumza mengi sana, na kabla sijafika kule, upako wote ulikuwa umenitoka kwa ajili yake. Kisha nikasema, “Vema, nitaenda tu kule na—na kuhubiri Ujumbe wa kuwaambia hao watu, ‘Msijipumbaze na madhehebu hayo’ na kadhalika na, ‘Tokeni, hivi.’” Na nilipofika jukwaani, huo ulikuwa umeniondoka. Sijui ilimaanisha nini, bali nilikuwa nikiendelea. Sijui.

⁶¹ Huenda ikawa ni mwisho wa safari yangu; huenda ikawa ni kuja kwa Bwana; huenda ikawa ni badiliko la siku, huenda ikawa ni kuja kwa huyo aliye mkuu, iwapo itakuwa mwingine mbali na yule amekwisha kuja tayari, huenda ikawa ni hiyo. Mambo hayo yote ambayo tumepata mifano yake, huenda yakawa ndiyo. Na ninaposimama hapa usiku wa leo mbele za Mungu na ninyi ndugu zanguni, sijui. Singaliwaambieni. Ningalijua, ningaliwaambieni, ama singetaja—singeleta jambo lo lote hivi kama sikujua ni njia gani... Siwezi kusema. Naenda sasa kwa mikutano pasipo chembe moja ya uongozi. Ninaenda kwa sababu sitaki kuketi hapa. Nataka kwenda mwituni kama mtu mwingine ye yote. Kama nimekosea kwa hili, Mungu anisamehe.

⁶² Kuna mambo matatu ambayo yangalinipata. Au ni mwisho wa safari yangu kusudi huyu mwingine apate kuja, nimefungua njia kusidi apate kuchukua madaraka kwa maana kumbukeni, yule atakayekuja kuhubiri atakuwa katika Neno, “Kuzigeuza imani za watoto ziwaelekee baba zao.” Huenda ikawa ni mwisho wa safari yangu. Huenda ikawa kwamba Yeye anabadilisha huduma yangu kurudia uinjilisti wa nchi za ng’ambo. Ama huenda ikawa hataniita tena kwa ajili ya uinjilisti, naye ananipeleka jangwani mahali fulani kunipaka mafuta kunituma kama “yule aliyeahidiwa” atakayekuja, nafikiri.

⁶³ Huenda ikawa moja ya mambo hayo. Siwezi kwenda jinsi nimekuwa nikienda. Kwa sababu mimi—watu wameniamini, si—sina budi kusema hivi (nasema hayo mbele ya mwanadamu). Watu siku nyingi hunichukua kama nabii. Sijichukui mwenyewe kuwa hivyo. La, bwana, sijichukui. Nime... sisemi hayo kuwa mnyenyekevu; nasema hayo nipate kuwa wa kweli. Sijichukui kuwa nabii wa Bwana. Si—sina heshima hiyo.

⁶⁴ Naamini ya kwamba Bwana amenitumia katika mambo madogo maalum kusaidea labda kuweka misingi kwa nabii atakayekuja. Lakini nabii hatendi ninavyotenda; sasa, mnajua

hivyo. Nabii si mwinjilisti, naye mwinjilisti si nabii. Bali Mungu ameweka kanisani, kwanza mitume, kisha manabii, halafu waalimu, ndiposa wachungaji na kadhalika. Mungu aliwaweka Kanisani kisha Mungu akawapa afisi.

⁶⁵ Bali asubuhi nilipoliweka hilo jiwe la msingi, kwa sababu (sasa, iwapo wewe ni wa kiroho utalipata)—kwa sababu ya kilio cha watu. . . Kama ungalivunja hilo ama uchukue hicho kitabu ukakisome, kilisema, “Fanya kazi ya mwinjilisti.” Hakuniita niwe mwinjilisti, bali, “Fanya kazi ya mhubiri wa Injili, kwa maana utakufa wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima, ila kwa—watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana maskio ya utafiti nao watajiepusha wasisikie yaliyo Kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.” Ona? Akaninukuulia Andiko hilo na kuniambia pa kulipata; kasema hayo mara tatu. Nami nikachukua Biblia na kufungua ambapo Yeye aliniambia, na ilikuwa hapo. Ndiposa mnajua habari za zile ndoo za Pentekoste ya Umoja na Pentekoste ya Assemblies, sikuzipitanisha kamwe. Niliupanda mti wao wenyewe mahali pale pale ulipokuwa, kwa maana naamini yote mawili yamekosea. Lakini kutoka kwao, nilikuwa msalabani mavunoni.

⁶⁶ Mungu huheshimu mtu ye yote aliye mwaminifu. Petro alisema hivyo; yeye alitambua kwamba Mungu hana upendeleo. Mataifa yote yalipozuru wakati—kwenye—katika nyumba ya Kornelio walipompokea Roho Mtakatifu vile vile kama wao walivyofanya hapo mwanzo. Ona? Mungu hana upendeleo. Tunamwona mtu akiwa mnyenyekevu sana na huku amekosea akali mnyenyekevu, bali kama yeye ni mnyenyekevu, Mungu atamwongoza Nuruni mahali fulani. Yeye ataifikia, maana Mungu anawajibishwa kufanya hivyo.

⁶⁷ Nasi tunafikiria kuhusu kule kuja kwa Bwana kukiwa jambo kubwa sana, na Ujumbe si zaidi ya ulivyoenenda; kumbukeni, kutakuweko kundi lililochaguliwa tangu awali litakalokuwa hapa Bwana atakaporudi, na huenda isiwe zaidi ya dazan. Ona? Hatujui, huenda ikawa milioni mia moja; huenda ikawa elfu kumi. Bali kama wale waliochaguliwa tangu awali watausikia Ujumbe na kuuamini, kama huu ndio Ujumbe uliotumwa na Mungu, ambao tunaamini ndio. . .

⁶⁸ Naam, sisi hawa hapa sasa, papa hapa hata mwisho wa wakati ambapo. . . Iwapo kweli Mungu aliniita (sasa sikizeni, hili halitarudiwa), iwapo Yeye aliniita kuwa Nabii Wake, basi bila shaka mimi sishikilii afisi yake. Manabii hawafanyi uinjilisti. Nabii hujificha jangwani peke yake pamoja na Mungu, hata anapopata moja kwa moja yale Mungu anayotaka afanye, naye hutoka moja kwa moja na kutoa Ujumbe wake, kisha anarudi jangwani tena. Yeye si mwinjilisti, akifanya mikutano na kuungwa mkono na mambo haya yote kama wafanyavyo wainjilisti. Yeye hafundishi kama wainjilisti. Yeye ana BWANA ASEMA HIVI, na hivyo ndivyo na ni hayo tu. Yeye analitoa,

analitupa, na kuacha chembe zianguke zinakotaka, kisha anaenda zake tena. Hamna anayejua aliko, yeye ametengwa mahali fulani.

⁶⁹ Sasa, siwezi...au...Iwapo yeye ameniita kuwa hivyo, siwezi kuwa mwinjilisti. Iwapo ameniita kuwa mwijilisti, siwezi kuwa nabii. Sasa, mnafahamu ninayokusudia? Sijui nifanyeje. Nilitenda kwa unyenyekevu aliponiambia hapo kwanza, juu ya mimi kushika mikono ya watu na kuwaombea, kisha kujua siri za mioyo yao, na mambo haya mbalimbali. Basi ndugu zanguni, hiyo haiwezi kukosea! Unajua hilo ni Kweli. Kila mmoja wenu anajua hilo. Ona? Na jinsi alivyoniambia ingesambaa ulimwengu mzima. Na imefanya hivyo, vivyo hivyo hasa. Kila taifa chini ya mbingu limesikia. Kila mahali—magazeti ya kila siku, kanda, kila mahali. Sijui jinsi hayo yalitendeka, bali kote ulimwenguni barua zinakuja na watu kutoka Thailand na Wahonttentots kule nyuma katika—jinsi hawa wamishenari wamelundikana kule na hizi kanda na kutoa hiyo tafsiri ya Neno. Na sasa, tunasikia kutoka ulimwenguni mwote (ona?), kote ulimwenguni. Sasa wao—Kanisa limechaguliwa tangu asili duniani kote, kila mahali. Wawili watakuwa kitandani, wawili makondeni. Ona? Mmoja atatwaliwa mwingine ataachwa.

⁷⁰ Sasa, kwa kuwa nimefanya kazi ya mwinjilisti (na haya ndiyo maombi yangu), iwapo inampendeza Mungu, nami nimefanya hiyo kazi sawa, nikitumainia ya kwamba nimempendeza Yeye, nikimwomba msamaha kwa ajili ya makosa yangu yote, basi huenda Yeye ananiita kutoka katika kazi ya uinjilisti nipate kuwa nabii Wake. Basi kama ndivyo ilivyo, nitaacha uinjilisti. Bali kama akiniita kuwa nabii, siwezi kuwa mwinjilisti. Iwapo nitakuwa mwinjilisti, siwezi kuwa nabii. Mimi ninachanganyisha afisi hizo mbili; hapo ndipo daima nimekuwa na wasiwasi. Kusimama jukwaani... Haijakuwa nzuri bado, haijafaulu. Mungu ameitumia, bali sijapata kuwazia ilikuwa mapenzi Yake ya moja kwa moja, imekuwa mapenzi yake ya kukubalia. Kusimama jukwaani, ono moja au mawili karibu yatakumaliza. Ona? Ndiposa kama utamwambia mtu huyu jinsi ya kujinyosha na jinsi ya kutenda; na mtu anayefuata yuasimama hapo, anatarajia jambo lile lile, nawe huwezi kumwambia isipokuwa Kitu Fulani kikwambie umwambie. Kisha huyo mtu mwingine anaona kama wewe ni msaliti na mtu aliyeanguka ama—ama—pepo ama cho chote kile kwa sababu hauwaambia yale wanayotaka kujua. Ona, hiyo siyo ile afisi—jinsi nabii anavyotenda kazi.

⁷¹ Nabii hukaa humu nyuma hata atakapoingia moja kwa moja hospitalini, ama po pote anapokwenda, akiwa na BWANA ASEMA HIVI na kusema hivyo na kurundi tena. Yeye si mwinjilisti kamwe. Yeye hafanyi mikutano na kujadiliana mambo, yeye yuna Neno la Bwana kwa ye yote aliyetumwa kwake.

⁷² Iwapo ametumwa katika Ikulu, yeye ataondoka kwenda moja kwa moja hata mbele ya Ikulu na kusema, BWANA ASEMA HIVI. Kama ni kwa Gavana wa jimbo, ye yote yule, ni BWANA ASEMA HIVI. Yeye hajipumbazi na kundi la makanisa, akijaribu kuwafanya waingie na kuchukua Neno, na kuhubri mambo haya kama wainjilisti, yeye si mwinjilisti.

⁷³ Kwa hivyo mnaona, ndugu zanguni, hiyo ndiyo sababu sijiiti nabii. Hata mimi siko katika afisi ya mmoja. Ona? Sasa mnafahamu ninayomaanisha? Sasa, kutakuwa na mengi yatakayoendelea hivyo kwa muda mrefu, lakini natumaini ya kwamba...sikuchukua wakati wenu mwingi sana, hata ninapoweza kupata Neno hili ndogo ninalotaka kusoma usiku wa leo.

⁷⁴ Sasa, ninafanya hivi. Sijajisikia kamwe ya kwamba inanipasa kuishi Indiana. Mimi ni—mimi ni mtambaaaji. Si... Nitaenda mahali pamoja na kuwazia, “Nitaenda humu na kuishi humu chini. Naam.” Siwezi kufanya hivyo. Ninapoenda mahali pengine mimi huwazia, “Nitaenda humu.” Ninapofanya hivyo...Mke wangu huniita (ni wimbo gani wanaouimba?) *Pepo Zisizotulia*. Mmeusikia, nadhani. Karibu ninyi nyote mmewasikia wakiimba...Vema, hivyo ndivyo anavyoniita, “Pepo zisizotulia.” Yapata wakati ninapofika hapo, nawazia, “Aisee, sina budi kwenda nyumbani. Sina budi kumwona mke wangu na watoto. Sina budi kwenda kanisani mara nyingine tena na kuhubiri.” Nifikapo hapa na kuhubiri mara moja, nikambusu mke wangu na kuwakubatia watoto wote, natoka nje uwanjani na kukata nyasi, kisha ndege inapita juu. Nasimama na kupangusa jasho usoni mwangu nami nataka kwenda pamoja naye. Yanipasa kwenda mahali pengine. Vema, nadhani sina budi kwenda kule chini, nami na—nashuka kwenda kule na kuhubiri kule wakati mdogo na kutazama huku na huko... Nyingine hiyo inapita juu, sina budi kwenda pamoja naye. Ona, hamna mahali pangu pa kupumzikia. Siwezi kufanya hivyo. Mimi situlii, nahamahama, mahali mahali...kitu fulani... Siwezi kujizuia. ni kitu fulani ndani yangu, nami najua sina budi kufanya hivyo.

⁷⁵ Sasa, kule kanisani katika hali yake sasa, ningesikia vibaya sana kuondoka humu. Nami nawaza kuwahusu ninyi nyote mnaoketi humu ambao naamini nitaishi Milele pamoja nanyi kule katika nchi ya utukufu. Tuna watu wazuri, watu bora, imara, watu wazima. Hivi majuzi tu, kulitokea ufufuo kanisani hapa kati ya watu. Roho akaja kati yao na akaanza kutoa karama. Nikayatazama hayo kuona kama yaishia katika ushupavu wa dini. Kila walipoanza kutenda hivyo, Roho aliyasahihisha na kuyarudisha. Naliwazia, “Bwana asifiwe.” Ona? Shikilieni tu mahali penu pale, hilo ni sawa. Ona?

⁷⁶ Sasa, mawazo yangu ni kwamba, ni haya. Ni...Kama ingaliwezekana ninapoaza kwenda mahali fulani...Sijui

ninakokwenda. Bali siwezi kutulia na sitakaa hapa. Siwezi kufanya hivyo. Inanipasa kwenda mahali fulani. Na labda sitakaa hapo ila siku chache kisha niende mahali pengine. Sina budi kwenda mahali fulani, sijui ninakoenda. Wala Ibrahimu hakujua alikuwa anaenda. Yeye alivuka tu mto akaanza safari. Hivyo tu.

⁷⁷ Naona kwamba kinachotupasa kufanya katika wakati huu. . . Naamini ya kwamba tunahitaji kanisa. Nafikiri—nafikiri Nyumba ya Mungu. . . Mnasema, “Vema, vipi. . . kuweka fedha hizo zote kwake iwapo Bwana yuaja?” Vema, itafaa nini kuweka fedha iwapo Bwana yuaja? Ona? Na iwapo watu wamefanya—walikusudia hizo fedha kwa kanisa, ni kazi yetu (kwa kura asili mia moja hapa nilizochukua usiku huo) kujenga kanisa; kwa hivyo lijengeni! Ningesema lijengeni! Naam, bwana!

⁷⁸ Sijasema haya hapo mbeleni, lakini ninataka kufanya hivyo mbele zenu ninyi watu. Sikutaka wanawake hapa, maana mmoja huegemea upande huu na upande ule. Naam, ninajaribu kuwaambieni sababu yangu ya kutaka kufanya hivyo. Nafikiri iwapo Bwana yuaja juma lijalo, hebu na tuanze kanisa juma hili. Bila shaka, hebu na tumwonyeshe Yeye. Hebuni tusimameni mahali panapotupasa. Naam, Bwana.

⁷⁹ Ndiposa kama sisi—kanisa litakapojengwa, naam. . . ? Tuseme kama Yeye. . . Vipi kama Yeye yu miaka kumi tangu sasa? Vipi kama yu miaka ishirini? Ama vipi kama Yeye yu miaka mia moja? Hata iwe nini, atakapokuja, hayo hayajalishi. Tunajua Yeye atakuja kwa ajili yetu wakati huo, kwa sababu hatuwezi tukaumaliza—miaka mia moja zaidi. Yeye yuaja kwa ajili yetu, bali hatuna budi kuacha kuachana nyuma yetu. Kisha nikawazia haya: basi mbona tusiache halmashauri ya kanisa hapa (nikinena kwao sasa) walijenge hilo kanisa? Waliweke humu; walitengeneze vizuri, na mahali pazuri ambapo watu wanaweza kuja.

⁸⁰ Ningeshauri Ndugu Neville awe mchungaji wa kanisa, mradi tu kanisa linamdokeza kuwa mchungaji; hiyo ni kura ya kanisa. Mradi tu anashikilia jukumu lake na anadumu katika imani na anataka kuja, anasikia uongozi wa Bwana; kisha uongozi wa Bwana kwake kukaa iwapo kusanyiko litakapiga kura hivyo.

⁸¹ Basi ningesema kila mmoja wa watu hawa nje hapa, watu hawa wengine, kama Ndugu Crase na Ndugu Junior na wengineo, mradi tu wanaona wajibu wao kazini mwao nao wanashirikishwa hapa pamoja. . . Huwezi kwenda kule chini na kukutana na Mmethodisti; huna ushirika pamoja nao. Wabatisti—ukianza kunena kuhusu kunena kwa lugha na ubatizo katika Jina la Yesu, watakutupa nje [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] upesi *hivyo*. Hiyo ni kweli. Unaketi kule, ungekuwa kama hu—hua miongoni mwa kunguru. Haungekuwa na ushirika kamwe. Utakufa. Siwafanyii mzaha

Wamethodisti na Wabatisti sasa, kumbukeni hilo. Sasa, sisemi hayo, mimi ninalinganisha tu. Kuna wengi wa hao Wamethodisti na Wabatisti ambao ni watu wazuri, wacha Mungu, bali ninanena kuhusu ushirika. Kuna Ndugu *Anaitwaje* kule nyuma usiku wa leo, yu—yule mwinjilisti anayeketi kule nyuma, Ndugu J.T. Parnell, Ndugu Beeler. Naamini Ndugu huyu anayeketi hapa... Baadhi yao... Wengi wenu hapa, watu wa Mungu, wito maishani yenu, mnaweza kuwa mkifanya jambo fulani. Msiketi tu kitako. Hebuni na tufanye jambo fulani. Msipopata ila mtu mmoja anayeokolewa, hebu huyo aokolewe—kila mmoja wetu...

⁸² Sasa, nafikiri kanisa hili... Kama ninyi watu mkitaka, mtakapolijenga kanisa hili, fanyeni hili kuwa makao yenu makuu naye Ndugu Neville hapa akiwa kama mzee mkubwa kati yenu. Ona? Na mara kwa mara mnapata swali ambalo hamwezi kujadiliana na kanisa lenu kule nje, basi lileteni hapa kwa ndugu Neville nanyi nyote mlizungumzie pamoja. Kama kuna... hamwezi kufikia uamuzi wo wote, nitakuja hivi karibuni, ndipo sote tutakutanika kwa ajili yake.

⁸³ Ndiposa mle ndani, wafanyieni mazoezi wahudumu wengine katika makundi yenu—watu ambao mnaona ya kwamba wana wito maishani mwao kwa ajili ya huduma. Wafanyieni mazoezi hao vijana; waleteni hapa kwa wazee. Nyote ketini pamoja katika mkutano wa wahudumu na humo mfundishe mambo ya Mungu yenye kilindi. Msiende upande mbaya. Wekeni mtu ambaye... mnayeweza kumwamini awe kama ki—kiongozi wenu. Kisha wakati mwingine kama hamuioni hasa jinsi anavyoiona, endeleeni—hiyo ni sawa; mko katika imani haidhuru, endeleeni tu. Labda tunapokutana basi, sisi sote pamoja, tutaomba; utambuzi wa Mungu utashuka, naye ataitoa jinsi ilivyo hasa (mnaona?) na atufanye tujue la kufanya.

⁸⁴ Na mle ndani, makanisa yanaweza kwenda kusikiza. Na kulizoeza kundi la watu... Na iwapo nimo katika kazi ya Uinjilisti mahali fulani, kuna mahali ninaweza kuwaweka ulimwenguni kote.

⁸⁵ Vipi kama nilikuwa kule India... nirudi India. Na huko ningewaambia watu hawa... Huenda ikawa wangekuwa na maelfu yao, nikae kule juma moja ama mawili, nao wangeona huduma hii; wangeipenda; wangeamini ni Kweli; wangetoka katika ukafiri. Ndipo nina... Na labda katika majuma mawili matatu... Nilipokuwa kule usiku muwili, na labda elfu mia moja wameokolewa na Kristo, hawana pa kwenda. Siku inayofuata nipande ndege nirudi kupitia Rumi, kisha Marekani, niwaache kama kondoo waliowekwa kati ya mbwa mwitu. Vipi kama ningalikuwa na kundi la watu, vijana waliofundishwa Ujumbe (ona?) kusema, “Sasa, ngoja kidogo; kabla sijaondoka hapa, hatuna budi kuweka makanisa haya katika taratibu. Nitampata mtu ambaye tayari nimempasha habari kwa simu;

nao wana pesa; wako njiani wakija hapa hivi sasa kuchukua hii—mtu mzuri. Kuna vijana wawili ama watatu pamoja naye watakaokuwa wasaidizi wake na wadogo wake.”

⁸⁶ Na kanisa la imani hii linaweza kuanzishwa pale ambalo litakuwa kanisa shirika katika India, kanisa shirika katika Ujerumani, kanisa shirika katika Uswisi. Hali hivi sasa, ingalitupasa kuwa nayo kote katika mataifa ambayo nimezuru. Na Ujumbe . . . kisha kutoka hapa kunakutoka lingine, kutoka lingine kunatoka lingine. Ona ninayomaanisha?

⁸⁷ Sasa, kesho usiku ama kesho kutwa, mtaona Mattson-Boze akija humu, ambaye ni rafiki yangu. Mtaona yale mtu mmoja, maskini Mswede aliyelemaa alivyofanya kule Tanganyika. Yeye alienda kule na . . . Sasa, Mattson-Boze ni mtu mzuri, bali yeye haamini imani tunayoamini sisi.

⁸⁸ Nimemchukua kule nje na kumchukua na kumfunga sana kwa Maandiko. Nikasema, “Mattson, wewe ni rafiki yangu. Sasa utaruka ama utakimbia; tutasimama hapa na kushikana mikono sisi kwa sisi kama ndugu Wakristo na kuzungumza.” Ona?

⁸⁹ Na nikaweka Ujumbe mbele zake naye angesimama tu pale na kusema, “*Nduku* Branham, wewe—wewe bila shaka unasema kweli.”

⁹⁰ Nikasema, “Sasa, Mattson, huamini hayo ama kweli ungaliyakubali.”

⁹¹ “Vema, *Nduku* Branham, na—naamini unayosema ni Kweli.”

⁹² “Basi mbona huyakubali?” Ona? Kuichomelea tu kwake naye—naye . . . Kisha mara tu aondokapo, ameenda. Ona?

⁹³ Bali tazameni yale mtu huyo alifanya katika misheni zake kule—mtu mmoja tu; maana yeye angalitumana moja kwa moja Chicago na kumchukua Burton na hao wengine wote, na kuwatuma kule hivyo na kuanzisha kazi hata sasa wanainuka katika makumi elfu ya ufufuo mmoja. Si mtu aliye na karama, ni mtu tu aliyekuwa na na ujasiri kuenda kule na kuanza. Mambo gani yangelitendwa chini ya hii? Wangefikia mamilioni. Hakika. Tumeupoteza wakati huo. Hivyo ndivyo shauri langu lingalikuwa.

⁹⁴ Sasa kumbukeni, katika kufanya haya utaona ya kwamba kutakuweco na wakati ambapo hautakubaliana na Ndugu *Fulani na Fulani*. Mtabishania humu. Basi kumbuka, mradi tu unafikia mahali unaposema, “Vema, kwa sababu yeye haamini jinsi nifanyavyo mimi, sitakuwa na . . .” Basi kuna kasoro kwako! Hamna shida na huyo mtu mwingine; wewe ndiwe una kasoro! Wakati ndugu wanaojaribu kushikilia pamoja . . .

⁹⁵ Kuna jambo moja, sisi jamaa ya Branham, tuko tisa nasi tunapigana kama mbwa wa kufugwa; bali hata hivyo, tunapomaliza kupigana, tungali tu jamaa ya Branham. Mmoja alijua huyo mwingine alikuwa Branham, nami nilijua

alikuwa Branham, naye alijua nilikuwa wa Branham. Ona? Bali tungepigana. Nanyi mnafanya hivyo katika jamaa yenu, bali wangali ndugu zako. Na hivyo ndivyo ilivyo. Huenda tukatofautiana (hiyo ni kweli), bali tungali mmoja. Sisi ni mmoja katika Kristo. Tunaamini Ujumbe huu na hebuni tukae nao.

⁹⁶ Nafikiri hivyo ndivyo itupasavyo kufanya kuzidi kuendelea hata Yesu ajapo. Na hivyo ndivyo nilivyotaka kusema katika hali hiyo. Nami naamini ya kwamba kama mngalikuwa na kama . . .

⁹⁷ Ona, hamna budi kuchochewa nayo. Iwapo hamjachochoewa, basi kuna kasoro. Kuna kasoro. Hamna budi . . . Si kusema tu, “Vema, mwezi uliopita nilichochoewa sana, bali sijui.” Ona, basi kuna kasoro mahali fulani. Hamna budi kuchochewa wakati wote (ona?) na uendelea tu kupigana; ni Shetani akijaribu kukupata . . . Kama vile daima nilivyompenda Rais wetu aliyetangulia, Bw. Eisenhower. Nilimpenda sana Jemadari Eisenhower. Yeye alisema, “Tulipokuwa tunapigana,” yeye akasema, “mara nyingi tumechukua risasi na kuishindilia kwenye bunduki na kulenga shabaha na kuiachilia, nayo ikafyatuka; haikupiga.” Kasema, “Hatukujisalimisha.” Kasema, “Huenda tuliweka nyingine nayo ikafyatuka pia.” Akasema, “Hatukukata tamaa.” Kasema, “Tuliendelea kuifyatua hata ikapiga.”

⁹⁸ Naam, hiyo ndiyo njia ya kushinda vita. Endelea kujaribu! Ingiza risasi na uilenge. Una kusudi—kulenga shabaha. Na iwapo haipigi, itupe kisha uingize nyingine, kisha ukajaribu tena. Iingize ndani kisha ijaribu tena hata moja itakapopiga. Kuna moja mle ndani iliyo hai. Na moja itapiga. Na hivyo ndivyo itupasavyo kufanya. Endelea tu kupiga, piga bunduki hata jambo fulani litakapotendeka.

⁹⁹ Ninafanya nini? Ninapiga bunduki sasa. Ninaenda nje hapa bila kujua hata—uongozi wo wote ama jukumu. Mamilioni ya watu wakikutazamia, “Utafanyaje? Hatua inayofuata ni gani?” Wengine wanadhani nimekufa; wengine wanawazia *hili*. Hata ile bunduki ilifyatuka hivi majuzi, nao wakasema nilikuwa nikijaribu kujiua—kila kitu. Ona? Kote nchini na kila kitu. Ona? Bali huna budi kukabiliana na hayo yote. Kisha una mzigu kwa ajili ya watu.

¹⁰⁰ Na hebu tu wazia vipi kama Mungu angaliweka juu yako ya kwamba ulijua mioyo ya watu uliokuwa ukiongea nao. Waza hilo! Ona, ndugu zangu, huenda ikawa . . . Najua mna mizigo, bali hamfahamu. Na mbali na hayo, hapa mna jukumu hapa . . .

¹⁰¹ Mnasema, “Vema, hiyo haina budi kuwa rahisi kwako, Ndugu Branham. Cho chote ufanyacho, Mungu hukuambia tu.” La, haniambii. Mimi huyatolea jasho tu kama mfanyavyo ninyi na hata zaidi. Hakika. Sina budi kuitolea jasho kuliko mnavyofanya, na mengi zaidi yatahitajika kwangu. Ambapo huna budi kujibu kwa ajili ya kanisa, ambapo huna budi kujibu

kwa ajili ya jamaa ama labda kwako mwenyewe (ona?), kuna mamilioni ya watu nitakaopaswa kuwajibia. Nami sina budi kujua nifanyavyo. Na iwapo Shetani anakuangushia mtu mmoja ama watu wachache ambao utawapata, na huku nje je, ambako watu wanaketi kwa taratibu? Basi anatupa vishindo vingapi humo? Ona? Kwa hivyo mna mambo mengi sana ya kukumbuka ndugu zangu. Hiyo... Si ajabu wakati mwingine napatwa na wasiwasi. Bila shaka.

¹⁰² Lakini sasa... Ninapigana sasa hivi. Ninaingiza risasi, kama ikipiga, basi. Kama haipigi, sitaondoka; nitatupa hiyo kama mshindo na kujaribu nyingine. Moja haina budi kupiga, hamna lingine. Moja ya hizo haina budi kupiga mahali fulani. Ndipo ninataka kuwa nikilenga shabaha, ili itakapolenga, itapiga kitu ninachopiga risasi. Nami... Mnajua ninayokusudia, nina hakika. Ona? Kuna kitu fulani mahali fulani. Ninaondoka kwenda kuhudhuria mikutano hii, kuchovya-chovyo kule ng'ambo; sina lengo la kufundisha mambo haya makuu ninayowafundisha enyi watu.

¹⁰³ Mnakumbuka ile ndoto niliyopata tafsiri yake ilivyokuwa. "Rudi ukakihiifadhi chakula." Ghala lilikuwa wapi?—maskani haya. Ni mahali gani nchini palipo kama hapa ambapo pangelinganishwa na ujumbe tulio nao? (Sasa, bila shaka, ndugu zetu hapa walio karibu hapa, makanisa haya mengine madogo, ni sisi. Sisi ni mmoja). Ungeenda wapi, kuupata? Onyesha mahali po pote panapoweza kulinganishwa napo. Ukienda moja kwa moja katika kanuni za kidhehebu, utaenda mbali sana na Jina la Bwana Yesu; utaenda mbali na mambo haya mengine. Ona? Na hapa ndipo chakula kimehifadhiwa.

¹⁰⁴ Vema Ujumbe mmoja niliowahubiria ninyi nyote... Tazama, nimekuwa nikiwahubiria kutoka saa moja hata masaa sita kwa Ujumbe mmoja. Vema, kama ingalinipasa kutumia mmoja wa Jumbe hizo, ningechukua juma moja kuchukua kidogo hapa na kidogo pale (ona?) kwa sababu umehifadhiwa.

¹⁰⁵ Uko kwenye kanda; utaenda ulimwengu mzima katika kanda ambapo watu manyumbani mwao... Hizo kanda zitaangukia mikononi mwa wale waliochaguliwa tangu awali wa Mungu. Yeye anaweza kuliongoza Neno; yeye ataelekeza kila kitu kuelekea njia yake hasa. Hiyo ndiyo sababu Yeye alinituma nirudi nikafanye hivi. "Kihifadhi chakula hapa." Alinikataza kwenda nchi za ng'ambo.

¹⁰⁶ Ndugu Arganbright alisema, "Vema, njoo; nenda. Nenda usiku mmoja bali tutakuzungusha ukaizuru nchi nzima—jinsi nilivyowaona Ndugu Fred na Ndugu Banks wakijaribu kwenda.

¹⁰⁷ Nilisema "Singalienda hivyo." Ilionyesha ya kwamba kulikuwa na jambo lingine. Nimekaza mwendo hata kuifikilia ile mede sasa, bali sijui niende njia gani. Bali kuna zana nyingi za vita zilizozunguka.

108 Je, Yeye aliniita nirudie uinjilisti? Ameniita nienda katika umisheni wa nchi za ng'ambo? Ameniita niwe nabii wake? Mimi ni mchungaji mahali fulani? Chochote kinipasacho kufanya, nitaendelea tu kushindilia risasi na kulenga shabaha. Moja itapiga! Bali sitakaa na kutazama na kusema, "Bwana, Wewe weka risasi katika bunduki." Nitaweka risasi katika bunduki na kulenga mimi mwenyewe. Hebu Naye apige bunduki. Ndiye atakayeshughulikia hayo. Hebu nami niendeleo kupiga hatua.

109 Kule nje ninakoenda kwenye mikutano hii sasa, ninaenda tu nje. Sijui, mi—mimi huenda nisiseme jambo moja kuhusu Jumbe hizi kama nilivyohubiri hapa. Huenda hata nisiwe na utambuzi wa usiku mmoja. Sijui. Mimi ninaenda tu, bila kujua ninayoenda kufanya. Singeliwaambieni, ninaenda tu.

110 Na hiyo ndiyo njia pekee... Na hivyo ndivyo ikupasavyo kufanya. Una jambo fulani moyoni mwako. Watu hapa wanataka kanisa. Lijengeni! Upesi mwezavyo, lijengeni. Pateni walimu wenu na kadhalika. Enyi ndugu kule pamoja na makanisa yenu nanyi mnataka ku—mnafanya kazi, Mungu atawapa thawabu kwa ajili yake. Nendeni kule! Hubirini! Fanya kila mwenzacho! Hebu ninyi nyote mkutane, enyi kundi hili la watu, mwe na mikutano na kuzungumzia mambo ya kindani ya Maandiko kisha mwombe. Msi—msije tu hapa pamoja isipokuwa mmekuja kwa ajili ya mkutano wa maombi pekee. Ombeni faraghani. Kaeni kule mahali hapo, ingieni katika vyumba vyenu, jificheni mahali fulani, kisha mpige magoti, na mkae mbele za Mungu na mkae pale. Kisha mkipata kujua, inaonekana kama kwamba kitu fulani kinainuka; lo, mnaenda tu, nanyi mnaona ya kwamba inaondoka kidogo kwa Neno, basi tahadharini! Haidhuru inaonekana nzuri vipi, komeni papo hapo! Roho mbaya aliwagusa, kwa maana Ujumbe wa wakati huu ni kwa Neno. Ona? Usi. . .

111 Ona, kama ukisema, "Jamani, Ndugu Branham, nakwambia hivi na vile. Nami, *fulani na Fulani* walisimama usiku uliopita, na jambo hili lingine likatendeka *hivi*." Itazame! Itazame kwa makini! Usikanushe lo lote. Ngoja tu uone jinsi inavyotenda kazi, kisha uilete kwa Neno uone jinsi inavyolingana na Neno. Kisha iwapo inalingana na Neno na kila kitu ni sawa, mshukuru Mungu na uendeleo tu mbele basi. Ona? Mradi tu inadumu katika Neno. Hayo ni maoni yangu, yale ninayofikiria mnapaswa kufanya.

112 Na Ndugu Neville, Ndugu Ruddle, Ndugu Crase na Ndugu Beleer nanyi nyote ndugu zanguni humu, "Junie," po pote mlipo na wengine wenu ndugu zanguni, Mungu awabariki sana. Namwona Terry, Lynn, Charlie Cox, David, wengi wenu vijana hapa, Mungu awatie mafuta. Jamani! Jinsi tungalitaka kuwachukua baadhi yenu muwe wainjilisti na kuwawekeneni mahali fulani (ona?), nikijua ya kwamba mmeinuka; mnaweza kusimama na kujua Ujumbe na kuusoma kujithibitishia

wenyewe. Iwapo unasikia wito maishani mwako... Nawaona vijana wawili au watatu, wanne au watano wameketi kwenye safu nyingine huku nyuma—na hivyo. Ninyi ni vijana wanaume; mimi ninazeeka. Ndugu Neville anazeeka. Sisi ni watu wa makamu. Kama wakati ukiendelea, tutaondoka jukwaani baada ya kitambo kidogo; hamna budi kupachukua mahali pangu. Ona?

113 Na kwa hivyo, mnaona... Ndiposa huenda ikawa katika siku hiyo hata itakuwa ikizidi kuwa kuu zaidi, iwapo kuna kesho. Bali mradi kuna leo, hebu na tufanye kazi ingali mchana. Kesho huenda isije kamwe. Ikija, na tuwe tayari kwake. Mnaona ninayomaanisha? Sasa hivyo ndivyo ningaliwawazia.

114 Je, haingekuwa vizuri ajabu kumwona Ndugu... kule juu kutoka Utica, Ndugu Crase, ninyi nyote ndugu mlio hapa mkiungana, mkutanike, mje mahali fulani; ninyi wahudumu mketi pamoja mzungumzie mambo. Hamna budi kuwa na ushirika mahali fulani. Hamna budi kuwa na jambo fulani la kuwakutanisha. Mkutanike pamoja kama kundi la watu na muamini ninyi kwa ninyi na mambo kama hayo, na kuzungumizia mambo haya na kupanga, labda mara moja kwa mwezi, wahudumu peke yao tu. Kutanikeni mahali fulani katika moja ya makanisa yenu. Ketini pale mkahojiane na kuzungumziana, kila mmoja wenu wachungaji, na wainjilisti, na ye yote yule. Na iwapo shida kubwa itazuka na hamwezi kuitatua, basi kama nimeitwa uwanja wa uinjilisti... Sijui kama nitaitwa; na iwapo nitaitwa, mnajua nitakuwa nikirudi mara kwa mara wakati wote. Ndiposa mkipata mambo hayo basi, nitakaporudi, naam, tutakutanika pamoja na kuketi kule. Iwapo mmoja wenu ana wito maishani mwako... Hatutakuwa na vitu kama mahojiano ya kibinafsi na mambo ambayo tumekuwa nayo, tutakutanika pamoja na kuketi kule hata tutakapokuwa na BWANA ASEMA HIVI.

115 Na iwapo unaweza kuwanyosha wahubiri naye apate kuendelea sawa, tazama atakayofanya. Yeye atawashawishi... Itashughulikia mamia ya mambo haya. Ndivyo ilivyo, tunapigania hayo, ona? Huna budi kuyaweka katika mpango fulani, mpango wa Mungu.

116 Kama Yethro alivyomwambia Musa, “Naam, huwezi kuyatatua yote.” Ama... Kisha Mungu akawaweka wazee kule, sabini, naye akaitoa roho iliyokuwa katika Musa na kuiweka juu ya hao wazee sabini kisha wakatabiri, na hiyo haikumfanya Musa dhaifu hata kidogo. Ilimtia nguvu. Yeye alikuwa na unabii mwingi ndani yake kama alivyokuwa nao kabla hawajaitoa roho kwake kutoa unabii. Ona? Yeye aliitenganisha, kasema, “Sasa Musa, hebu wao wahukumu mambo madogo na—bali inapofikia mambo yaliyo muhimu, wewe kutana nao na uwasaidie hivyo.”

117 Sasa, njia ndiyo hii. Hiyo ndiyo iliyokuwa njia ya Mungu kule nyuma; hiyo ndiyo njia ya Mungu katika—katika wakati wa kanisa la mwanzoni, nami naamini ya kwamba ndiyo njia ya Mungu sasa (hiyo ni kweli) kwetu kufanya hivyo. Kwa hivyo hebu na tufanye hivyo. Hivyo tu. Tunaweza kufanya hivyo kwa neema ya Mungu. Hamuamini hivyo?

118 Sasa, hebuni. . . Sasa, hebu tuone. Lo, nimekwisha kuchukua wakati wangu, bali. . . Billy aliandika maandishi hapa. Hebu kidogo, nami nitaona ni nini: “Nimetoka New Albany. . . binti, Grace. . . Hospitali ya Memorial. . . aliuvunja mguu wake. . . nataka aombewe. . . Tr-o-u-b, W.C. Troub—Troub” (kitu kama hicho). Hebu na tumwombe huyu. Bibi mdogo.

119 Baba yetu wa Mbinguni, tunapoongea sasa. . . Nami nawazia ya kwamba labda wakati Irenaeus alipoangalia kundi lake ndogo la watu, labda lilikuwa ndogo kuliko lililoko hapa usiku wa leo. Nao hawakuwa na mahali pa kuketi. Wao waliketi kwenye kipande baridi cha mwamba wa kale, nao waliketi pale naye akawazungumzia. Hao watu wakaondoka, hata wakati wa kuondoka kwao ulipowadia, wao walijua wangelishwa simba, vichwa vyao vingalikakwa. Bali ile “imani ya baba zetu ingali hai bado, mbali na vifungo, moto na upanga.”

120 Nakushukuru kwa ajili ya watu hawa, Bwana. Naomba ya kwamba utawabariki. Sasa, mbariki kila mmoja wao katika Jina Lako, upate kuwadumisha katika imani iliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu, kusudi wao wasiiondokee kamwe. Na kutoka kwa kundi hili hebu uwatume wachungaji, waalimu, wainjilisti. Ee Mungu, tujalie. Hebu na washikilie ngome kila mahali, po pote walipo. Hebu na waendee kufanya kazi hata Yesu atakapokuja.

121 Na sasa, Baba, naombea kila moja ya haja hizi ambazo zimeletwa hapa usiku wa leo na naomba ya kwamba utamkumbuka maskini bibi huyu humu, ambaye ameuvunja mkono wake. Hebu nguvu za Mwenyezi Mungu zimponye na kumpa afya. Tujalie, Bwana. Naomba ya kwamba utamsaidia na kumbariki. Mbariki mpenzi wake kwa kupiga simu. Na zile nguvu zilizomfua Yesu kaburini zimwinue msichana huyu. Na mkono wake upate afya.

122 Mahitaji haya ambayo yalitajwa usiku wa leo: maskini kijana huyo anayeketi pale aliye na hii. . . Nilimsikia ndugu akitangaza hayo, ya kwamba ule ugonjwa wa Hodgkins umemla hata uso wake umechomwa na madini ya radium na vitu wanavyompea. Mungu, mrehemu mvulana huyo, hebu na aishi. Tunawazia kuhusu mtu huyo ambayo hakujitayarisha kukutana Nawe na amekwisha ondoka sasa. Mkewe amevunjwa kichwa, mtoto waliyemfanya mwana. Na hawa wengine wote. Dada Bruce akibeba hayo maji, yeye anazeeka, Baba. Huyu hapo amechoma mikono yake, na kote mwilini mwake.

Tunamwombea. Huenda ikawa amewekwa hospitalini, nasi tunaomba ya kwamba wewe ungempa afya na apate kutoka. Tujalie, Baba. Tunaomba baraka hizi katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

¹²³ Sasa, nataka kuwaulizeni jambo fulani. Na kuwaulizeni iwapo—iwapo mnaamini ya kwamba tuna wakati kwa ajili ya Neno ndogo. Mnao? Kwa... Sasa, ni... najua imechelewa kidogo, bali nilikuwa na jambo ndogo hapa nililowazia hivi leo ambalo ningetaka ku—kunena juu yake kwa muda mchache, na huenda likawasaidieni. Nami nilidhani kwanza kwamba ningetangaza haya. Sasa, imo katika kanda hii, na iwapo mtu ye yote angalitaka kurejea kwake kamwe, Jim atakuwa nayo. Ona? Kwa yale nafikiri yanapaswa kufanywa. Na sasa yale yanayopaswa kufanywa kwa—kwa ajili yenu enyi ndugu.

¹²⁴ Sasa, je, mnajua wakati hao watu wa zamani walipoondoka, wakati mwingine kulikuweko tu na yapata watu sita ama wanane wote pamoja—nao waliitikisa nchi. Vema, mnajua wakati Akila na Prisila, ufufuo huo mkuu ambao Apolo alikuwa nao kule, kulikuweko yapata watu sita ama wanane wanaume kwa wanawake katika kundi hilo. Kanisa hilo lote lilimaanisha sita ama wanane. Mna mara tano au sita, mara saba zaidi hapa usiku wa leo kama walivyokuwa nao wakati huo.

¹²⁵ Mnajua Yesu alikuwa na wanafunzi kumi na wawili tu. Kila mara sisi huwazia juu ya hizo hesabu kubwa. Ni katika makundi haya madogo ambayo Yeye huipata. Mnaona? Tazama kote kote katika nyakati, wakati wo wote alipowahi kukutana na mwanadamu, ilikuwa katika makundi madogo (ona?)—naye akanena nao na kuwaagiza. Ni mapenzi mema ya Mungu kufanya hivyo; hivyo ndivyo anavyotaka kufanya. Na sasa, tunataka tu kumweka Mungu kati yetu na tuende tukafanye mambo haya.

¹²⁶ Sasa, Jumapili asubuhi, Bwana akipenda, nataka kuzungumza nanyi juu ya *Uinjilisti wa Wakati wa Jioni*. Kisha, nita... Bwana akiniruhusu, huenda nikaondoka hata majira ya mwisho wa mwaka huu na... kabla ka... kabla sijarudi tena. Nami labda nitarudi yapata—yapata Septemba. Na sasa, ninatarajia yapata wakati huo ya kwamba kila kitu kitaendelea vyema kabisa kwa ajili yenu ndugu, na mikutano yenu itaongezeka, na neema ya Mungu itakuwa juu yenu hata tutakapoonana. Nami ninatumainia ya kwamba mtaniombea nipate kufaulu. Kumbukeni, ni—maombi yenu kwangu... Hiyo ni kusema nyinyi ni wezangu, ninyi ni rafiki wasiri wangu, wasaidizi wangu; na sote pamoja sisi ni wasaidizi katika Bwana. Na sasa, ninaposimama kule mbele ya maadui, nataka kuwakumbuka hao askari wa kweli na waaminifu ambao maombi yao ya wagojwa na walioteseka hujibiwa, na hao watu wananiombea. Mimi ndiye ninayeyahitaji kule nje. Mi—mimi

kweli ni mhitaji, kwa hivyo nyote niombeeni mtakapokusanyika. Msinisahau katika kila mkutano; niombeeni.

¹²⁷ Sasa, katika Yohana sura ya 9, nataka kusoma kutoka kifungu cha 26 hata cha 35. Sasa, kwa muda mchache halafu tuta—tutafunga katika dakika ishirini ama thelathini zijazo, ama labda kabla ya wakati huo, Bwana akipenda. Sasa, nataka kusoma Maandiko haya sasa kutoka Yohana Mt. 26 hadi—Yohana Mt. 10-9:26-35, nimeandika hapa chini, jambo nililokuwa nikiwazia.

Basi wakamwambia, Alikutendea nini? Alikufumbua macho jinsi gani?

Akawajibu, Nimekwisha kuwaambia, wala hamkusikia, mbona mnataka kusikia tena? Ninyi nanyi mnataka kuwa wanafunzi wake?

Basi wakamshutumu wakasema, Wewe u mwanafunzi wake yule; sisi tu wanafunzi wa Musa,

Sisi tunajua ya kwamba Mungu alisema na Musa; bali yule hatujui atokako.

Yule mtu akajibu, akawaambia, Hii ni ajabu! Kwamba ninyi hamjui atokako, naye alinifumbua macho!

Twajua kwamba Mungu hawasikii wenye dhambi: bali kama mtu ni mcha Mungu, na kufanya mapenzi Yake, humsikia huyo.

Tokea hapo haijasikiwa ya kuwa mtu ameyafumbua macho ya kipofu, ambaye alizaliwa hali hiyo.

Kama huyo asingalitoka kwa Mungu, asingeweza kutenda neno lo lote.

Kisha wakajibu—Wakajibu, wakamwambia, Ama! wewe ulizaliwa katika dhambi tupu, nawe unatufundisha sisi? Wakamtoa nje.

Kisha . . . Yesu akasikia kwamba wamemtoa nje; naye alipomwona alisema, Wewe wamwamini Mwana wa Mungu?

¹²⁸ Sasa, ningetaka kuzungumza kwa dakika chache nanyi ndugu, nikijua ya kwamba mazungumzo yangu madogo hapa (sijui yatakuwaje), nikitumai ya kwamba Mungu atayatumia kwa njia fulani, na sasa katika hii, juu ya Neno Lake . . . Kwa hivyo najua hayo Ndugu Sink. Ndugu Neville, ama mmoja wenu wahudumu mnaohubiri kwa kawaida. Na ninapokuwa hapa pamoja nanyi, mimi—kama mtanisamehe, ningetaka tu kuwazungumzieni tu kwa dakika chache kwa njia hii.

¹²⁹ Sasa, nataka kuchukua somo hapa juu ya *Kuwa Upande wa Yesu*. Mafarisayo na viongozi wa siku Zake kila mara walijaribu kumvunjia njina mbele za watu. Hiyo ilikuwa tu njia aliyokuwa nayo Shetani ya kufanya kazi. Mafarisayo wote

pamoja na walimu wa siku Zake daima walijaribu kumvunja jina Yesu. Wao... Takataka zote walizoweza kumtupia, walifanya hivyo. Wao walimchunguza daima kuona ambapo wangelipata kosa, nao hawakuzungumzia mambo Yake mema, kila mara walikuwa wakitafuta kitu cho chote ambacho wangelimvunja jina kwacho na kusema, “Mnaona, tazameni hapa. Angalikuwa mtu wa Mungu, hangalifanya hivyo” ama, “Angalikuwa mtu wa Mungu, hangalifanya hivyo.” Walikuwa wakijaribu kumtupia uvuli kusudi watu wasimwamini. Hiyo ni kazi ya Shetani, na njama hizo za kale hazijakoma kamwe.

¹³⁰ Kuna wakati mwingi ambapo muhudumu atafanya kosa. Na akija katika mtaa huo, ndugu mpendwa anayejaribu kufanya yaliyo kweli na kuwaongoza watu kwa haki, kila kitu ambacho Shetani anaweza kumwelekezea asiyeamini ama anayedai kuwa Mkristo katika mtaa huo kumtupia mtu huyo, yeye atafanya hivyo. Mnajua, njia halisi ya Kikristo ni kuficha kila uwezacho kutoka kwa ndugu. Usiseme mambo yake mabaya; sema tu mambo yake mazuri. Sema tu yale unayojua kumhusu ambayo ni mema. Kama cho chote ni kibaya kiache. Maskini mtu huyo ana mengi kutosha dhidi yake haidhuru. Usijaribu kuchukua ufito ukamsukumizie mtu huyo upande wa ndani sana wa shimo. Msimamo wa Mkristo ni kumtwaa na kumtoa shimoni. Ona? Usikajaribu kamwe kumpiga kikumbo. Yuko chini tayari. Jaribu kumsaidia aamke. Kisha... Bali wengi wetu sana siku hizi, watu wengi sana leo, huenda nikasema, hujaribu kufanya hivyo. Kama wangelipata jambo fulani ambalo wangelisema ambalo lilikuwa baya sana...

¹³¹ Sasa kwa mfano, kama—kama mmoja wenu ndugu angelifanya kosa na kufanya jambo baya—ambalo unaweza kufanya; mimi pia, kila mmoja wetu. Bali tunapoendelea, hebu na tukumbuke sisi ni ndugu. Na iwapo tuna vita vyo vyote, hebu tupigane sisi kwa sisi. Vileteni pamoja. Vileteni mbele ya ndugu zetu mkavisuluhishe.

¹³² Naam, ilikuwa kwamba katika jamaa ya Branham, kama mmoja wa hao watoto alifanya jambo fulani, wangemwambia Bill juu yake, maana mimi ndimi niliyekuwa mkubwa. Nami ilinibidi kusimama pale na kuona ni nani aliyekuwa asiye na hatia na ni nani mwenye hatia. Vema, uamuzi wangu ulikuwa ya kwamba kama wao... ni nani kati yao hana hatia na ni nani mwenye hatia, kisha kama bado hawakuamini hilo, basi walirudi nyuma yangu na kupigana kisiri. Bali hata hivyo wao walikuwa wangali ndugu. Mnaona? Wao wangepigana nyuma ya nyumba wao kwa wao na kupigana mbele ya nyumba wao kwa wao. Kwa hivyo, hivyo ndivyo ilivyokuwa (ona?), na i—tungali ndugu.

¹³³ Vema, hivyo—hivyo ndivyo i—inatupasa kufanya haya. Ona? Kama una neno dhidi ya mtu fulani, ndugu yako, usimwambie mtu mwingine juu yake kama ni kosa; nenda kwake

ukamwambie. Ndipo iwapo atabishana nawe, basi mchukue mtu mwingine mwende naye. Kisha ifanye jinsi Biblia ilivyosema.

134 Bali Yesu, wao—wao walijaribu kupata kila kivuli kidogo wanalikipata kujaribu kumvunjia jina mbele za watu. Na hivyo ndivyo Shetani anavyotaka. Wao wanataka ku—wao wanataka kudhuru ushawishi wako mbele ya watu. Ndipo unatakiwa kuangalia unayofanya. Tembea kama mtu halisi wa Mungu, nena kama mtu wa Mungu. Ona? Tenda kama mtu wa Mungu, ishi kama mtu wa Mungu, kwa sababu Ibilisi, mshitaki wenu, anazunguka-zunguka kama simba angurumaye akitafuta kumeza awezacho.

135 Mbona wao walifanya hivyo? Walimwonea wivu. Hiyo ndiyo sababu walijaribu kumvujia jina. Wao walionea huduma Yake wivu. Hiyo ndiyo sababu wao walikuwa wakijaribu kumvunjia jina. Bali Yeye alikuwa na huduma ya Mungu nao walijua hivyo, bali ilikuwa kinyume cha kanuni zao za imani; kwa hivyo walikuwa wakijaribu kumvunjia jina. Kufanya kila kitu Yeye—kila kosa ndogo ambalo wangepata, kumwondolea mbali. Walimtaka aondoke; walitaka watu wamshutumu. Walitaka kusema, “Sasa, mtu huyu si kitu. Tazameni hapa. Sasa, ndiye huyo, ye—ye—yeye alifanya hivi. Na mnajua hiyo si haki. Tumefundishwa maishani mwetu mwote ya kwamba inatupasa kuwaamini wazee. Naye ndiye huyu hapa, alisimama hapo na kumpigia huyo mzee kelele. Yeye hakukubaliana na mapokeo ya wazee, nasi tumekuwa—nasi inatupasa kuamini mapokeo ya wazee wetu. Tumefundishwa hayo na kila rabi miaka hii yote. Naye huyu mtu hapa anakuja na kutokukubaliana nao.” Ona? “Naam, mtu kama huyo hapaswi kuwa mhubiri.”

136 Ona, wao walikuwa wakijaribu kumvunjia jina. Bali katika hayo yote, wale waliomwamini Yeye na kumpenda na walikuwa wameona ishara Zake za kimiujiza na kimaandiko hawangekwazwa nao. La, bwana! Hao waliomwamini Yeye walimwamini. Wale waliompenda walisimama pamoja Naye. Hawangeona yale hao wengine waliyowaonyesha.

137 Lo, laiti tungalikuwa hivyo. Laiti hatungaliona. Mtu fulani akija hapa na kusema, “Wajuaje? Wao husema u Mpetekoste.”

“Si kwa dhehebu.”

138 “Vema, wewe—ulikuwa—wewe ni mmoja wa hao wanaobatiza katika Jina la Yesu.”

“Naam, hiyo ni kweli.”

“Vema hebu niwaambieni jambo fulani. Namjua mtu aliyebatizwa hivyo na akafanya *hivi na vile*.”

139 Bali tazama, hilo halihusiani nalo kamwe. Ni Shetani akijaribu kukutupia uvuli. Wao daima wanajaribu kukuonyesha merikebu ya kale iliyovunjika pwani, bali hawakuonyeshi ile iliyofaulu. Hiyo ni kweli. Ona?

140 Wao daima wanajaribu kutupa chambo cha kunguru kule na kusema: “Huu ndio mfano; hivi ndivyo ilivyotendeka. Lo, namjua mhubiri fulani ambaye ni mhubiri wa Utakatifu naye alifanya hivi, vile, au vinginevyo.” Bali hawaneni habari za wengine ambao hawakuwa wa Utakatifu waliofanya vivyo hivyo pia. Mnaona? Nao hawakuonyeshi mambo makuu ambayo Mungu amefanya.

141 Kama alivyosema mtu fulani: “Lo, mtu huyu alikosea sana. A—alikosea sana.” Huenda alifanya hivyo. “Alijiangamiza; alifanya vibaya sana; alifanyika mshupavu wa dini.” Huenda alifanya hivyo. Bali wanapoonyesha ni wangapi wa—waliofanya mambo mabaya sana, na hawa mamilioni ambao hawakufanya vibaya hivyo, je? Walikosa kuona hayo. Ona ninayomaanisha?

142 Kwa hivyo hao watu walijaribu, hao Mafarisayo, na Masadukayo, na wanafiki, na Maherodia, na kadhalika walijaribu kumfunika Yesu uvuli; lakini hao waaminio wa kweli, wale waliochaguliwa tangu awali kuusikia Ujumbe huo, waliusikia na hawakuona kosa lolote ndani yake.

143 Vivyo hivyo sasa, wale wanaomwamini Yeye wanampenda; wale wanaomwamini Yeye hawaoni kosa ndani Yake. Hawaoni uzushi wote; hawaoni kosa lo lote; hawaoni kosa lo lote katika Neno Lake; hawaoni kosa lo lote kwa watu Wake; wanamwona Yesu na hilo latosha. Wao wame—wamechaguliwa kwa Uzima wa Milele, kwa hivyo walienda upande wa Yesu na kukaa pale.

144 Tulikuwa tunaimba wimbo mdogo, Ndugu Roy Roberson na...tulikuwa tunauimba wimbo mdogo hapa, nadhani ni wakati wewe ulikuja hapa:

Ningetaka kufuatana na watu wachache wa
Bwana waliodharauliwa;
Nimeanza pamoja na Yesu, na nitafaulu.

Afadhali niende na Yesu Peke Yake,
Nami nipate mto kama ule wa Yakobo, jiwe.

145 Umesikia huo wimbo mdogo. Vema. Afadhali nichukue njia ya kutokupatana, nichukue njia ya waliodharauliwa, nichukue njia ya wanaosengenywa, na nitembee pamoja na Yesu. Nisione hatia yoyote. Nisione kosa la mtu mwingine, nishiye njia tu. Hilo tu.

146 Sasa, hivyo ndivyo walimfanyia Yesu. Hawaku—hawaku... Na lazima mwafunze watu wenu, nyinyi wachunganji, kufanya vivyo hivyo. Ikiwa mtu atakuja na kusema, “Aha—a—a wajua, kanisa lako, wako *hivi na hivi*. Wao si... .

147 Naam, bwana, huenda kukuwa na watu dazan moja wanaoketi hapa wakati uo huo, lakini vipi yule mtu mmoja aliye sawa anayeketi pale? (ona?) Wewe hu—wewe hauwezi kuona

misitu badala ya miti, hilo tu. Ya—ya kwamba inajirudia tena. Waona sasa?

148 Na kwa hivyo, wao walijaribu. . . Hawakuwa tayari kukubali kuwa Yeye alikuwa akitenda kazi ya Mungu, kwa hivyo walikuwa wakijaribu kupanda kuhitilafiana watu wasije wakaamini; lakini hao watu waliomwanimi Yeye walikaa Naye; walimfuata.

149 Wajua, nilifikiri hapa. . . Baadhi ya watu ambao nimewaandika hapa chini. . . Yule kipofu hangalibandilishwa nao, yule mtu aliyekuwa amemfungua macho; twajua ile hadithi. Aliwapa swali kali sana. Sasa, walipanda wakaja kule; kisha Yesu akapitia hapo, naye alikuwa mtu aliyedharauliwa na kuchukiwa. Biblia ilisema atakataliwa; hakuwa na umbo hata tumtamani. Na sisi kama kondoo tumepotea. Alikuwa mtu wa huzuni, ajuaye sikitiko. Na yote ambayo Biblia ilisema Yeye atakuwa. Atadharauliwa na kukataliwa. Na sisi twaona mtu huyo.

150 Sasa, wale walioliamini neno, walijua kwa yale mambo yale Yesu alikuwa akiyatenda na mambo ya maisha Yake yalivyokuwa; walijua Yeye alikuwa nani. Kwa hivyo hawakuweza kuweka dhara yo yote juu Yake, kwa sababu hawakuiona. Na wajua, upendo ni upofu hata hivyo kwa mambo hayo; upendo hufunika dhambi nyingi, mwajua. Upendo mkamilifu huondosha woga, na dhambi, na ugomvi wote; upendo hufanya hivyo.

151 Sasa, huyu kipofu alikuwa ameketi hapo, na Yesu na wanafunzi Wake wakapitia pale; na nafikiri Yesu aliwapa somo dogo hapa. Walipomwona huyu mtu maskini na kipovu, walifikiria, “Vema, sasa hakika, kuna dhambi nyuma ya hayo mahali fulani.” Tukiona jambo fulani likitendeka kwa mtu fulani, kila wakati twasema, “Vema, yeye alitenda dhambi; alitoka katika mapenzi ya Bwana mahali fulani.” Ndugu Crase alisema kweli kabisa, yeye alitoka katika mapenzi ya Bwana mahali fulani katika wazo la mtu fulani. Wakati bunduki iliponilipukia, “Vema, yeye alikuwa nje ya mapenzi ya Bwana.” Ndugu Neville akapata ajali ya motokaa, “Yeye alikuwa nje ya mapenzi ya Mungu.” Hilo si kweli hasa. La, bwana sivyo, ilivyo, Mungu huruhusu mambo hayo.

152 Yesu aligeuka akawafunza wao somo. Walisema “Hapana budi babaye alitenda dhambi au mama yake alitenda dhambi au ni yeye alitenda dhambi?” Yesu akasema, “Hapana hata mmoja wao aliyetenda dhambi, bali kazi za Mungu zidhihirishwe.” Amina! Mwaona? Mungu huacha mambo yatendeke ili—ili kazi za Mungu zidhihirishwe.

153 Sasa, kwa hivyo Yeye akasema—kamwambia yule mtu na kufungua macho yake, kisha yeye akaenda zake. Na hapa wakaja Mafarisayo wakati jambo hilo lilipovumishwa huko.

Hapa kuna mtu aliyekuwa kipofu, ameketi kule chini anaomba msaada; na hapa anaweza kuona. Na huo ulikuwa ni uvumi miongoni mwao, na ee jamani, hilo lilichochea kitu fulani! Ndio hawa hapa wanakuja, na wakaona kuwa yule kipofu anaweza kuona. Na kwanza wao walienda—walitaka kutafuta njia fulani ya kuwaogopesha watu wote, sababu walikuwa tayari wamesema, “Ikiwa mtu ye yote atafuata fundisho hili jipya na nabii huyu mpya anayeitwa Yesu wa Nazareti, moja kwa moja waturudishiwa makaratasi yao na ushirika kutoka kanisani. Atatengwa na sinagogi. Ukishirikiana naye, uhudhurie mojawapo ya mikutano yake au cho chote kile, hauwezi kuendelea tena.”

154 Kwa hivyo walitaka kufanya wonyesho mkubwa juu ya hilo, kwa sababu walimchukia Yeye. Hawakuwa wanafikiria juu ya mtu huyo kipofu, lakini walikuwa wanataka kufanya wonyesho mkubwa ili wafanye watu wasimkaribie.

155 Wao walisema walitaka kuwauliza baba yake na mamaye; kwa hivyo wakaenda wakampata baba na mama. Wao walisema, “Huyu ni mwana wenu?”

Yeye akasema, “Naam, bwana.”

“Alizaliwa kipofu?”

“Naam, bwana.”

“Basi a—amepataje kuona?”

156 Na baba na mama waliogopa, Biblia ilisema, sababu walijua watatengwa na sinagogi ikiwa watakubali kwamba . . . Waona, hapo Yeye alishushwa chini. Wao walisema, “Sasa, twajua huyu ndiye mwana wetu.”

157 Ee, labda watu elfu chache walikuwa wamesimama hapo. Lakini kama yeye angali . . . kama hao Mafarisayo walionuka waliweza tu kuharibu Jina Lake pale au kufanya jambo fulani kuwatisha watu hao, wangalimfukuza pale katika mkutano ule. Mnaona? Ushawishi Wake wote ungalipotea.

158 Kwa hivyo walisema . . . Wakaja kundi nzima hapa na mavazi ya kikuhani wakasema, “Nena kwa niaba yake.”

159 Wao walisema, “Tunajua huyu ndiye mwana wetu; tunajua alizaliwa kipofu, lakini jinsi aonavyo mimi sijui. Mwulizeni yeye mwenyewe; yeye ni mtu mzima.” Ona?

160 Vema. Kwa hivyo wakaenda wakampata. Kasema, “Nani alikufanya upate kuona? Alikuonyaje wewe?”

Akasema, “Mtu mmoja anayeitwa Yesu wa Nazareti alinifumbua macho.”

161 Wao wakasema, “Msifu Mungu.” Kasema, “Naam, tunajua mtu huyu ni mwenye dhambi.” Ki—kisha kasema, “Anatoka wapi Yeye?”

¹⁶² Yeye akasema, “Mimi sijui. Yeye alipitia hapa tu akaniponya, na hayo tu ndiyo nijuayo. Ninajua... Jambo moja ninalolijua. Siwezi kuwaambia habari Zake kwamba ni mwenye dhambi au la, mimi sijui, nilikutana na mtu huyu hivi leo tu. Lakini ikiwa—ikiwa Yeye anaweza kunipa mimi ku—kuona kwangu, mimi najua neno hili moja, kuwa ingawa mimi nilikuwa kipofu, naweza kuona sasa. Nina hakika kwa hilo, kwa kuwa nilikuwa kipofu nusu saa iliyopita; na sasa nina macho mazuri sana kama ye yote wenu enyi watu, kwa hivyo mimi najua naweza kuona.”

¹⁶³ Ee, ni mwiba jinsi gani kwao! Kwa hivyo wakafikiri, “Mbona...”

¹⁶⁴ Yeye akasema, mbona akasema, “Ninyi nanyi mnataka kuwa wanafunzi Wake?” Hilo ni nzuri—huo ni ushuhuda mzuri na imara. Huo ni mzuri—huo ni msingi mzuri. Huko—huko ni kushuhudia bora sana; nionavyo mimi.

¹⁶⁵ Kasema, “Ninyi nanyi mna...” Hapa kuna mshiriki wa kawaida, kipofu, akisimama barabarani baada ya kukutana na Yesu, sasa anauliza wanafunzi—anauliza hao Mafarisayo kama wanataka kuwa wanafunzi Wake—hao maskofu, viongozi. “Mnataka kuwa wanafunzi Wake pia?”

¹⁶⁶ Walisema, “Hasha, Wewe u mwanafunzi Wake; Sisi tu wanafunzi wa Musa (watazama kule nyuma katika historia, mwajua). Sisi tu wanafunzi wa Musa. Mtu huyu, hatujui lo lote kumhusu yeye; hatujui mahali anakotoka. Vema, hatuna fununu ya mojawapo ya shule zetu aliyowahi kupitia. Hakuja kamwe kutuuliza sisi kuhusu mambo haya. (Waona?) Hatujui lo lote kuhusu hili. Nyinyi watu huko, mwatambua ya kwamba mtu huyo hajatiwa mikono? Mtu huyo ni mpiga ramli au kitu fulani; yeye ni Beelzebuli. Nyinyi mnalogwa. Mbona, yeye hana mamlaka; hatujampa yeye bado. (Mwaona?) Hata hatujui alikotoka mtu huyu.”

¹⁶⁷ Maskini kijana huyu aliyesimama hapo na angeona akasema, “Sasa, hii ni ajabu.” Waona, yuko karibu anaanza kuwashinda watu, hawa Mafarisayo, kuwafanya waogope. Waona? Lakini alikuwa tayari yuko upande wa Yesu. Waona? Basi akasema “Hii ni ajabu.” (Acha nifafanue baadhi ya maneno ambayo huenda alisema) “Sasa, ninyi watu hapa mmekuwa mkiendesha mambo yote ya kidini hapa kwa miaka mia kadha, na—ninyi munanena kuhusu Masihi atakayekuja na jambo fulani litakalotukia katika vivuli vya wakati, ambapo Mkombozi yuaja kutuona. Kisha mnatuambia ya kwamba Yeye ajapo—ajapo—yote atakayofanya. Na hapa, ninyi, viongozi wa kiroho, makuhani wakuu, na makuhani wa huu umma, mnasimama hapa pamoja mbele za watu hawa, mkijaribu kumharibia Jina, mkijaribu kunena jambo ovu dhidi Yake; na mtu huyu amekuja na akafungua macho yangu yaliyopofuka... Nilizaliwa kipofu. Baba yangu na mama yangu wako hapa kutoa ushuhuda kuwa

mimi nilizaliwa kipofu, nimekuwa nikiketi hapa kati yenu kwa miaka hii yote—nilizaliwa kipofu. Na hili halijafanyika tangu mwanzo wa ulimwengu. Na hapa Mtu fulani anaweza kuja na kufanya muujiza ambao haujawahi kutendwa tangu mwanzo wa ulimwengu; na ninyi, viongozi wa kiroho, hata hamjui lo lote kulihusu!” (Whiu! H—m—m—m!) Kasema, “Mimi nasema hii ni ajabu.” Alichagua upande wa Yesu. Waona.

¹⁶⁸ Aliruhusiwa kuwa kipofu ili kazi za Mungu zipate kudhihirishwa (ona?), sababu alikuja upande wa Bwana Yesu. Aliungana Naye.

¹⁶⁹ Sasa yeye aliwaehoma wao kwa mwiba. Unajua walivyofanya? Wao walisema, “Sasa, tunajua wewe ulizaliwa katika dhambi. . . unajaribu kutufundisha. . .” Wakamtenga na kanisa; kamtoa nje, wakamwondoa yeye nje, waka mtupa nje. Lakini mara baada ya kutupwa nje, umepata kutambua? Yesu alimpata tena! Amina, amina! Yesu alimpata tena. Kwa hivyo usiwe na huzuni, iwapo watakutupa nje. Yeye atakupata tena. Waona? Vema.

Kisha akamwambia, “Wewe unaamini Mwana wa Mungu?”

¹⁷⁰ Yeye akasema, “Bwana, Yeye ni nani.” Hata yeye hakujua, lakini jambo la pekee alilojua, ni kwamba ingawa alikuwa kipofu, aliweza kuona wakati ule.

¹⁷¹ Nami najua jambo moja, ndugu zangu. Huenda wakauita, huu ushupavu wa dini na cho chote watakacho; bali ingawa wakati mmoja nilikuwa mwenye dhambi, ni—ninaingia katika neema sasa. Jambo limetendeka kwangu. Ona? Na—najua neno hili moja, kwa kutumainia Neno Lake, kwa kumwamini Yeye. . . Nimetengwa na kila dhehebu chini ya uso wa mbingu. Hamna hata moja ambalo lingenipokea tena. Mnajua hivyo. Watu wengine watafanya hivyo, huku nje, watu wazuri—watanikubali; bali kila dhehebu, linanidharau. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Bali Yeye amekwisha nipata; Yeye atanipata mahali fulani. Hiyo ni kweli. Kuja hivyo. . .

¹⁷² Na kwa hivyo itakuwa sawa, kwa maana tunataka kuchagua upande wa Yesu, na njia pekee unayoweza kuchagua upande wa Yesu ni kukubaliana na yale aliyosema, kuamini Neno Lake. Kwa hivyo hebu na tuchague upande Wake. Yule kipofu aliwatolea ushuhuda halisi. Vema.

¹⁷³ Tunaona tena wao walijaribu kuharibu Jina Lake. (Kwa muda mfupi tu, nami yanipasa kuruka mambo mengine hapa kwa hivyo. . .) Wakati mmoja kulikuweco na Mfarisayo. Nilihubiri juu ya hilo hapa wakati mfupi uliopita na kuuita *Kutawadha Miguu ya Yesu*. Naamini nyote mlinisikia nikihubiri huo hapa, wakati Mfarisayo alimwalika Yesu nyumbani kwake—Maskini mzee Mfarisayo aliyekuwa mgumu sana—akamwalika. Na mnajua niliifanyia mchezo wa kuigiza, jinsi yule tarishi alivyomkuta, Naye akashuka akaja; hata

ingawa Yeye alijua alikuwa amedharauliwa, hata hivyo alienda haidhuru. Nao walipomwingiza mle, hawakuitawadha miguu yake ila walimwacha aketi pale, huku ananuka na kadhalika kwa ajili ya uchovu wa barabarani, naye akaketi mle.

¹⁷⁴ Kisha akaja maskini mwanamke mmoja. Wao wakawazia, “Lo, jamani, Bwana ni mwema kwetu, kwa sababu ona, hii inaleta tu karamu yetu kuu...” Wao walikuwa wamemleta kule kumfanyia tu mzaha. Wao walimleta mle kusudi wapate kumdhihakiki. Na sasa, wao walifikiri Bwana alikuwa akitenda pamoja nao; kwa sababu huyo mwanamke malaya mwenye tabia baya alikuja kule na alikuwa analia na kumtawadha miguu kwa machozi yake na kuipangusa kwa hii nywele. Maskini Mfarisayo na hao wazee wengine wakisimama kule pembeni walisema, “Ndugu, kila kitu... Bwana aliyapanga hayo kwa ajili yetu hasa. Hapa tunaweza kumharibia jina sasa hivi. Yeye anajiita nabii, nao watu wamdhani kuwa nabii. Nao wanamwita nabii wa Galilaya. Naye hata anadai kuwa Masihi, nasi tunajua ya kwamba huyo Masihi atakuwa Nabii. Naye ndiye huyu hapa ameketi kule nyuma. Mnaona kule tulikomleta. Angalieni kule. Jamani, tumemnasa hivi sasa! Ndiye huyo ameketi kule nyuma, amejikunyata kama mtoto wa mbwa aliyepigwa ama cho chote kile kule nyuma, na malaya wa tabaka yake anakuja na kuitawadha miguu yake hivyo. Na sasa, hata hajui. Kama angalikuwa nabii, angalijua huyo alikuwa mwanamke wa namna gani. Sasa, enyi vijana, tutanywea hili divai,” kasema, “kwa maana tazameni hapa...”

¹⁷⁵ Ona, kila kitu kuliharibu Jina Lake, cho chote kile kuangamiza matumaini ya watu, bila kujua ya kwamba hao walikuwa wamepagawa pepo kufanya hivyo. Wao walikuwa wakifanya kazi na ibilisi, wakijaribu kuharibu Jina la Mwana wa Mungu.

¹⁷⁶ Je, wao walifanyaje hilo, ndugu? Kwa sababu hawakuyachunguza Maandiko. Yesu alisema, “Mwayachunguza Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa Milele ndani yake na hayo ndiyo yanayonishuhudia.” Lo, jinsi alivyokuwa na huduma kuu! Ona? Naam, bwana. “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini.” Ona?

¹⁷⁷ Bali hapa huyu Mfarisayo, akasema, “Tumempata sasa. Lo, tazama hapa, huenda ikawa kuna watu elfu moja mia tano hapa kwenye karamu hii. Sasa mtazame ameketi kule. Ndiye huyo pale ameketi pamoja na kahaba!”

¹⁷⁸ Na lo, jamani, lilikuwa jambo baya vipi siku hizo! Whiu! Hm-m-! Naye alikuwa pale pamoja na mwanamke mwenye tabia baya, alijipenyeza mle kama—ilionekana kama alijipenyeza. Yeye alimpita mtumishi mwanamume na kadhalika na kuketi pale.

179 Naye akasema, “Ndiye yule pale akimtawadha miguu yake. Basi, kama yeye angalikuwa nabii. . . Mnaona, ndugu zanguni, mtu huyo si nabii kamwe. Angalikuwa nabii, basi angalijua ni mwanamke jinsi gani aliyekuwa anamtawadha miguu.”

180 Naye Yesu akaketi na kumtazama, hakujongeza mguu hata alipomaliza. Iwapo utamfanyia Yesu jambo fulani, Yesu ataketi akikutazama ukitenda wakati mwingine. Yeye huacha uendeleo hata utakapomaliza, kisha dhawabu inakuja. Labda utapiga mbio maishani kote ukimfanyia kazi, bali usijali, kuna dhawabu mwishoni ukichagua upande Wake.

181 Huenda usione hata mtu mmoja ameponywa aliyemwombea; endelea tu kuwaombea. Nimesema mara nyingi, “Kama nikiombea mia tano usiku huu; hao wote mia tano wawe wamekufa asubuhi, usiku wa kesho nitahubiri uponyaji wa Kiungu na kuwaombea wangojwa.” Ona? Haina uhusiano wo wote nao. Ona?

182 Atakuacha ushuke moja kwa moja chini na kadhalika, hata utakapofikia kikomo cha safari yako na kumaliza kazi yako, kama alivyomwachilia huyo mwanamke. . . Yeye alitaka kumtumikia, kwa hivyo Yeye aliunyosha mguu Wake pale na—na kumwacha aitawadhe. Lo, kama angalisema, “Usifanye hivyo,” yeye angaliruka juu na kutimua mbio; bali Yeye alimwacha amtumikie.

183 Alipomaliza, alipomaliza huduma aliyokuwa afanye, aliinua macho yake akamtazama huyo mnafiki aliyekuwa amesimama pale nyuma, aliyekuwa akijaribu kuharibu Jina Lake, kasema: “Simoni, nataka kukwambia jambo fulani; si huyu mwanamke, bali wewe. Wewe, unayesimama nyuma kule, moyoni mwako hiyo ndivyo sababu ulinileta humu. Haushiriki pamoja Nami. Sikujua? Bali ulinileta humu, kisha ukaniketisha hapa nyuma kusudi unidhihaki. Hebu. . .Haukunipa maji kuitawadha miguu yangu; haukunipa cho chote cha kuniburudisha. Mimi nikaketi hapa huku nikiwashwa na kusikia uchungu, haukunipa mafuta nijipake uso. Uliona haya kunibusu ukinikaribisha au kunisalimia kwa mkono. (Ona?) Uliona haya mbele ya wenzio; uliona haya kufanya hivyo. Mwanamke huyu, tangu aingie humu, hajafanya lo lote ila kunipangusa miguu Yangu na kuiosha kwa machozi ya macho yake, akaipangusa kwa kitambaa cha nywele zake. Basi nitakuonyesha tu kama Mimi ni nabii au la.” Amina! Napenda hilo.

184 “Basi, nataka kukuzungumzia kwa muda mfupi tu. Umesamehewa dhambi zako ambazo ni nyingi.”

185 Hm-m-m, je, wao waliharibu Jina Lake? Wao walidhania ya kwamba walikuwa wamefaulu, walidhani walikuwa wamesha ikomesha; walidhani waliisha mshinda kusudi ufufuo Wake usipate kuweko katika jamii hiyo; walidhani wamekwisha

kuangamiza ushawishi Wake, bali ilichukua tu mtu mmoja aliyempenda kubadilisha hali hiyo yote!

186 Unajuaje iwapo wewe siwe huyo mtu katika jamii yako kwa mtu mtakayekutana naye? Chagua upande Wake; mtumikie; mtumikie; mnajua ninayomaanisha, ndugu zanguni? Kuwa upande wa Yesu. Mchukue...Mfanye ndiye chaguo lako. Mtumikie haidhuru kama mtu ye yote...au kama utalipwa ama cho chote kile. Haijalishi. Ngoja hata hiyo kazi itakapokwisha.

187 Ungetakaje Yeye aseme...Hata ingawa ulikuwa umewaombea wagojwa nao hawakupata afya; ingawa uliomba upate kunena kwa lugha, na hukunena; uliomba upate kutoa unabii, haukufanya hivyo; hata hivyo, jambo ambalo tu unaweza kufanya ni kusimulia hadithi ya Yesu kanisani mwako, ama katika jamii yako, kazini mwako. Haukufanya hata jambo moja; haukumwongoza hata mtu mmoja. Mwanamke huyo hakumwongoza hata mmoja kwa Kristo, bali alimtumikia. Na ina tofauti gani mwishoni mwa safari, iwapo Yeye atasema, “Nami nakwambia, dhambi zako zote...Hata kama huenda ikawa hamna hata ombi moja lililojibiwa, bali ulikuja kwa msimamo wa Neno Langu. Ulikuwa kwa sababu uliniamini, nawe ukanitendea kazi. Nami nasema ya kwamba tayari umesamehewa dhambi nyingi ambazo umetenda.” Hilo lingekuwa nzuri kutosha kwangu! Amina. Naam, bwana.

188 Vema. Wao wanataka kusema, “Siku za miujiza zimekwisha” na—na kadhalika. Hebu waendeleo kusema hivyo, bali hebu sisi tumfanyie Bwana Kazi. Wao walimdharau kwa sababu walimwonea wivu. Hiyo ndiyo sababu pekee; wao walimwonea wivu. Wao walikuwa wakijaribu kuharibu ushawishi Wake mbele za watu vivyo hivyo wanavyofanya sasa. Wao...Iwapo wanaweza kuharibu ushawishi wa Ujumbe mbele za watu, basi wamekwisha shinda kitu hicho. Hiyo ni kweli. Kwa sababu... Kwa nini walijaribu kufanya hivyo?—Kwa sababu Yeye alipinga kanuni zao zote za imani, na kila kitu walichoamini; na kuita imani zao—imani zao zote na kadhalika...Yeye alipinga hayo yote; nao walimchukia, kwa sababu Yeye hakuungana nao.

189 Sasa, kama angalikuja na kusema, “Lo, Kaiyafa, mtu wa ajabu sana wa Baba Yangu, Mimi ndiye Masihi. Njoo hapa, Kaiyafa. Unaona yale maji pale? Unakumbuka kule Misri, Musa, yule nabii mkuu, aliyageuza yakawa—yakawa damu. Unakumbuka hayo, Kaiyafa?”

190 “Lo, kijana, ninaijua hadithi hiyo sana.”

191 “Vema, Kaiyafa, nitayageuza maji sasa, toka maji yawe damu, kuwaonyesheni ya kwamba mimi ndiye yule Nabii ambaye Musa alinena habari zake. Ndiyo hayo, Kaiyafa. Wasemaje kuhusu hilo?”

192 “Waonaje kuhusu Kaiyafa akiwa Mfarisayo? Waonaje kuhusu Mfarisayo?”

193 “Jamani, nafikiri hao ni tabaka nzuri sana ya watu. Lo, ninyi nyote mnashika mapokeo ya wazee vizuri sana.”

“Unajua, huenda ikawa ndiwe Masihi.”

194 La, hangalikuwa! Hiyo ingekuwa ishara dhabiti kwamba Yeye siye. Unapooni mtu akija na kusema, “Njoo hapa, nami nitawaonyesha nitakayofanya.” Kisha, “Njoo hapa, nami nitafanya *hivi* na *vile*.” Kumbukeni tu ya kwamba sasa hivi kuna hila fulani kwake kwanza. Yesu alisema, “Sifanyi neno lo lote hata Baba anionyeshe kwanza.” Ona?

195 Naam, Yeye alikuwa anawapinga; alifundisha dhidi yao. Alihukumu kuweka kwao kwa Sabato; alilaumu jinsi wao walivyovalia mavazi; Yeye alilaumu namna zote za maisha yao, mapokeo yao yote, kuosha kwote kwao kwa midumu na birika na kuosha kwa kila kitu. Yeye alihukumu hayo kabisa. Kwa kuvalia nguo zao, Yeye alisema, “Ninyi huvalia mavazi yenye mapambo na kutaka vitu vya juu na kufanya sala ndefu na kukula nyumba za wajana.” Kasema, “Mtapokea hukumu zaidi.”

“Vema, kumbuka, mimi ni Daktari *Fulani* . . .”

196 “Sijali wewe yu nani.” Masalale, Yeye aliwakemea kweli kweli. Wao hawaku . . . Kwa nini?—kwa maana wao hawakumwamini Yeye; Yeye alikuwa Neno. Ona? Alikuwa akijaribu kuvunja hilo kundi la wafuata sheria, na kama Yeye alikuwa humu dunia leo, angejaribu kufanya jambo lile lile.

197 Watu wengine husema, “Vema, hebu ngoja kidogo. Sisi huadhimisha Sabato. Daima . . . Sisi hufanya *hivi*. Nanyi mwajua, tunaadhimisha *haya* yote, na kuadhimisha *yale*, na kila . . . Naam, kila Ijumaa Kuu . . . Naam, wakati wa kufunga unapowadia, siku arobaini kabla ya Pasaka, kila mara sisi huadhimisha Kwaresima. Mimi huacha kuvuta sigara kwa muda wa siku arobaini. Huacha kunywa pombe siku arobaini hapo mbeleni—wakati wa Kwaresima.” Lo! Mapokeo ya wazee—wanaofuata sheria. Ukimpenda Mungu, wewe—hutavuta sigara kwanza. Ukimpenda Mungu, wewe . . . Niliandika nyuma ya Biblia yangu, ya kwanza niliyopata kuwa nayo kamwe; nikasema:

Usiniulize maswali ya kipumbavu;
Azimia hili moyoni mwako.
Nampenda Bwana kwa moyo wangu wote,
Usivute sigara, kunywa pombe, ama—usivute
sigara, kutavuna tumbaku, ama kunywa
kileo cho chote.

198 Hilo lingali hivyo leo. Sifanyi hivyo kwa sababu nafikiri Yeye atanihukumia kufanya hivyo; singeacha kufanya hivyo kwa sababu ni jambo ovu na halimpasi muhudumu. Hiyo ni kweli. Singesema . . .

¹⁹⁹ Wakati mwingi mimi huenda manyumbani na kuna wanawake wamesimama kule. Nami naenda kwa hiyo nyumba na kupiga mlango na dada fulani angekuja mlangoni na kusema, “Ingia, Ndugu Branham.” Iwapo mumewe hakuwa humo, mi—mimi—isipokuwa iwe ni mambo ya ugojwa na kuna mtu mwingine aliye pamoja nami, siingii. Ndiposa, wao wataniita hospitalini ama chumbani, kasema, “Ndugu Branham, njoo huku. Mimi ni Dada *Fulani* kutoka mahali *Fulani*. Niko humu mkahawani. Ni—nilimleta mama yangu; yeye ni mgojwa.” Ningemchukua mke wangu. Kama sifanyi hivyo, ningemchukua ndugu mwingine.

²⁰⁰ Ona si—mimi si—sifikiri. . . Nafikiri ingekuwa sawa kwangu kwenda kule, bali vipi kama mtu fulani aliniona nikiingia mle? Ona? Vipi kama mtu ye yote aliniona nikifanya hivyo? Ona? Basi muda si muda, wao wangesema, “Aliingia mle alimokuwemo huyo mwanamke. Anamwadama mwanamke huyo.” Hiyo. . . Ona, hilo lingekuwa jambo ambalo sipaswi kutenda. Ona? Usifanye jambo kama hilo kamwe, maana unaweka jiwe la kujikwazia mbele ya mtu mwingine. Ona? Siamini ya kwamba ningefanya jambo lo lote baya mle. Haingekuwa—singeweza—kumtumainia Mungu kuingia mle. Haidhuru jambo hilo lilikuwa nini, ningemtumainia Mungu. Bali hata hivyo, mnaona, ndani—ndani. . . Nampenda Bwana vizuri kutosha hata singalifanya hivyo. Ona, ni upande ulio nao. Wewe—hufanyi hivyo kwa sababu ni jukumu lako kufanya hivyo; unafanya hivyo kwa maana unampenda Bwana. Si lazima ufanye hivyo, bali unafanya hivyo haidhuru.

²⁰¹ Paulo aliniambia, “Vitu vyote ni halali kwangu, lakini si vyote vifaavyo.” Ona? Paulo angalifanya mambo mengi sana ambayo alijua Bwana alimfahamu na kumwamini, bali haikufaa kwake kuyafanya. Kwa hivyo hivyo ndivyo hawa wanaotii sheria, wanajaribu kusema, “Siku arobaini kabla ya Pasaka kila mara tunaanza kufunga.” Nao wanakula kiasi wanachokula kila mara. Labda wao wanasema, “Vema, sipendi maharagwe, kwa hivyo sitakula maharagwe wakati wa Kwaresima.” Nimewasikia wao wakisema. “Sipendi nyama ya nguruwe, kwa hivyo sitakula nyama ya nguruwe, mwajua.” “Mimi sitakunywa wakati wa Kwaresima.”

²⁰² Mwanamke mmoja aliniambia, kasema, “Unajua niliyoacha kwa ajili ya Kwaresima mwaka huu, Ndugu Branham?”

Nikasema, “La, uliacha nini?”

²⁰³ Kasema, “Peremende.” Kasema, “Sijapata kuijali sana, hata hivyo.”

²⁰⁴ Ona? Basi. Sasa, wao wanaita huko kufunga. Ona?—Utii wa Sheria. Wao husema, “Vema, nina. . . Mnajua, ni—ni—nimeyumba-yumba kanisani muda mrefu, maana. . . Nawaambieni, nilihudhuria shule ya juma pili mwaka mzima,

kwa kuwa mwalimu wangu alisema kwamba—watatoa Biblia kwa yule ambaye hatakosa hata siku moja.”

²⁰⁵ Sasa, Ndugu, hivyo ndivyo inavyotendeka. Afadhali niende nikajinunulie Biblia. Ona? Kama huendi kanisani kwa sababu unampenda Bwana, afadhali usiende. Hivyo tu. Ona? Kwa maana... Unaenda kule kwa sababu unampenda Mungu. Nawazia huu wimbo tunaouimba;

Kibarikiwe kifungo
Kitufungiacho mioyo;
Ushirika wetu wa fikira zetu
Ni kama ule wa mbingu.”
Tutawanyikapo mbali
Hiyo yatufadhaisha;
Bali tungali pamoja rohani
Hata tutakutanika.”

²⁰⁶ Ona? Naam. “Tutawanyikapo mbali, hiyo yatufadhaisha.” Nimeuona wakati, ndugu zanguni (hebu nisihukumu sisi, lakini hebu tu nifanye tuamkie jambo fulani), nimeona wakati ambapo kanisa hili, ambapo ilipowabidi watu kungoja hata juma tano kukutana wao kwa wao, wangelia juu yake. Hiyo ni kweli. Nimeuona wahudumu wakija hapa na kusema, “Uhali gani?” Vema, watu hao wana moyo mmoja. Ona?

²⁰⁷ Wao wanakutana mlangoni na kusema... Hao akina dada wanakutana wao kwa wao kule nyuma na kukumbatiana wakisema, “Dada, usisahau kuniombea sasa, Kipenzi. Nitakuona tena Jumatano usiku. Utaomba, sivyo? Niombe; nitakuombea.” Wakifanya hivyo, na machozi machoni mwao.

²⁰⁸ Unaona hao ndugu wakisalimiana kwa mikono na ilikuwa vigumu kuachana hivyo. Huo ndio ushirika wa Kikristo. Ona? Ona, wakingoja tu, wakiombeana. Naam, bwana. Hivyo ndivyo inavyotupasa kuwa. Vema.

²⁰⁹ Sasa, watu hawa waliofanya matamshi haya, hawakuwa watu wabaya. Hawakukusudia kuwa waovu; walidhani wao wanamtendea Mungu kazi. Hao Mafarisayo na kadhalika, hawakuwa watengenezaji wa pombe ama walevi; wao walikuwa watu wa kidini. Hawakuwa watu wabaya; wao tu—wao hawakukubali Neno la Kweli. Wao hawakumkubali Roho. Kwa nini? Walishikilia kanuni zao za imani na mapokeo ya viongozi wao. Ona? Inaonyesha ya kwamba wao waliwapenda viongozi wao.

²¹⁰ Ndiye huyu Kaiyafa mkuu, yule kuhani mkuu; ndio hao pale makuhani wengine mashuri. Na watu hao wanaenda... Sasa, wachukue Wakatoliki, wao... (Si kuwatupilia mbali, vivyo hivyo Waprotestanti.) Mchukue Mkatoliki; yeye anampenda kasisi wake. Na—nami nitamwambia kuhusu Neno la Bwana, naye anaona kazi ya Mungu. Atasema, “Bali—bali kanisa langu haliadini hayo.” Halafu aondoke akiongea na kudhulumu,

sasa asema . . . Mwanamke aliniambia hivi majuzi, kasema, “Ni dhambi kwangu kukusikiza.” Ona? Yeye hakutaka kuwa mtu mbaya. Yeye alilipenda kanisa lake sana pamoja na kasisi wake hata kama angalisikiza kitu kingine cho chote . . . Yeye alikuwa mwaminifu kwa huyo kasisi.

²¹¹ Mashahidi wa Yohova ni waaminifu kwa yale wanayoamini; Wabatisti ni waaminifu kwa yale wanayoamini; Wapresbeteria ni waaminifu kwa yale wanayoamini, nao ni waaminifu sana kwa wachungaji wao . . . Je, sisi hatuwezi kuwa waaminifu hivyo kwa Neno? Ona? Sasa, kama hao . . .

²¹² Nataka kuwaulizeni jambo fulani. Mnasema, “Vema, Ndugu Branham, wajuaje kwamba si waaminifu?” Sasa, iwapo hao Mafarisayo na Masadukayo na viongozi wa siku hizo wangiacha kanuni zao za imani na mafundisho yao ya sharti na kusikiza yale Neno lilivyosema na vile Yesu alivyokuwa anawaambia (Jinsi hasa Masihi alivyopaswa kufanya), wangelimshikilia. Ona? Bali waliwapenda sana viongozi wao . . . Wao hawakuwa watu wabaya. Hawangaliiba, kudanganya, kulaani, mambo kama hayo; hawangalifanya hivyo. Hawangefanya uzinzi. Naam, sivyo kabisa. Naam, hao wangelishuhudia kupigwa mawe kwa mtu aliyetenda jambo kama hilo. Nao hawangali—hawangalifanya hivyo. Walikuwa watu wazuri, bali jambo lilikuwa kwamba, wao hawakuwa watu wa kiroho. Kwa uadilifu, walikuwa sawa, lakini hayo siyo yaliyo muhimu. Na Yesu aliwaambiaje? Hata kwa hao watu waaminifu, Yeye Yeye alisema, “Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi.” Ona? Neno ndilo muhimu.

²¹³ Sasa, nitaharakisha upesi niwezavyo. Naam, wao hawakuwa wamejazwa Roho, bali wao walikuwa waaminifu na walishikilia kanuni za kisasa za imani za viongozi wao. Ona? Vema. Huduma Yake ilikuwa ikichongea mafundisho yao. Hilo ndilo jambo muhimu. Sasa, tazama! Sasa, hebu ichukue tu . . . Sasa, hebu tu . . . (Ndugu zanguni, nitawaulizeni mnisamehe hivi sasa kwa kuwachelewesha hivi. Mimi—mimi . . . Labda hamtanitaka nirudi tena kwa mwingine, bali tazameni, sikizeni haya. Ona, nawatakeni mhakikishe mnalipata hili).

²¹⁴ Sasa, wao walikuwa na kanuni zao za imani, nayo yalikuwa makanisa makuu na watu mashuhuri na watu wakuu—watu watakatifu, watu wazuri, watu wanyenyekevu, watu wema, watu wenye heshima, waungwana, wenye elimu, werevu, wa kidini—sivyo? Sasa, sote tunajua hivyo. Wazuri kama wote wale ambao ungaliwapata mahali po pote. Ona? Bali Yesu alipokuja, huduma Yake ilichongea mafundisho yao, maana Mungu alikuwa akidhihirisha kwa huduma ya Yesu Kristo ya kwamba Yeye alikuwa pamoja Naye.

²¹⁵ Je, Petro hakunukuu jambo lile lile? Yeye alisema, “Enyi waume wa Israeli, na ijulikane kwenu ma mkasikilize maneno

yangu.” Akasema, “Yesu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu.” Ona? Ona, kama wao . . .

²¹⁶ Kama alivyosema huyu kipofu, “Si hii ni ajabu? Ninyi ndio viongozi wa kiroho taifani, na hapa yuaja Mtu akanifumbua macho kwa nguvu za Mungu, wala hata hivyo hamjui lo lote juu Yake.” Yeye alisema, “Hii ni ajabu.” Yeye alikuwa na jambo fulani, sivyo? Bila shaka. Vema. Alifanya . . . Mtu ambaye angefanya hivi, hata hivyo wao hawakujua alikotoka! Naam, hii ni ajabu.

²¹⁷ Sasa, tazama siku hizi, ndugu zangu. Ona, tuna . . . tunajua ya kwamba tuna mwongozo wa Mungu. Tunajua unafanya miujiza; unaponya wagonjwa; hata unafufua wafu; unatoa pepo; unanena kwa lugha na kufasiri lugha; unatoa unabii; yanatendeka; Yeye alitufasiria ndoto, kufasiri kukamilifu, halisi kabisa. Basi si ajabu ya kwamba viongozi wakubwa wangesema tulikuwa kundi la wenda wazimu na huku wao ni viongozi wa taifa, viongozi wa makanisa? Hiyo ni ajabu.

²¹⁸ Ni nini? Ingali ni wivu. Roho na Nguvu na Neno la Mungu katika siku hizi za mwisho zinachongea mafundisho yao ya sharti na kanuni zao za imani (ni hivyo tu kwake) hata wamewapofusha watu kwake. Kwa hivyo, ndugu zangu, mlilo watoto, ninyi nyote mnaoenda humu, makanisa haya, shikilieni Neno la Mungu. Msijongee. Iwapo huwezi kulifanya litimie, msimzuie mtu mwingine. Simama kule huku unabisha mlango, ukilielekezea tu. Hiyo ni kweli. Dumu pale pale. Usianzishe uzushi wo wote, kwa sababu utakuchongea tu. Hiyo ni kweli. Lakini ukidumu wa kweli na mtakatifu kwa Neno hilo, Mungu atakuthibitisha. Hiyo ni kweli.

²¹⁹ Huduma Yake ilikuwa ikichongea mafundisho yao na mafundisho yao ya sharti, kwa hivyo walichukua kila nafasi ya kumwangamiza waliyopata. Kila kitu ambacho wangepata, wapate kumwangamiza, walifanya hivyo. Wakijaribu kusema, “Vema, sasa tazama hapa . . . *fulani na fulani* . . . Huyu.”

²²⁰ Yeye anaketi pale siku moja katika nyumba ya Simoni mwenye ukoma. Hamna neno lililosema kwamba Yeye alimponya. (Yeye alikuwa mwenye ukoma). Halisemi kwamba Yeye alimponya. Hiyo ni kweli.

²²¹ Yeye alipitia kwenye birika ya Bethsaida na kulikuweko yapata watu elfu mbili walioketi pale, viwete, vipofu, vilema, waliopooza. Naye akamwendea mtu mmoja akamponya kisha akaondoka. Kasema, “Vema sasa, kama Yeye alikuwa Masihi, Yeye angaliwaponya wote. Kama alikuwa amejaa huruma kama nyote mnavyosema amejaa, Yeye angaliwarehemu wote.” Kila walichopata kumtia alama nyeusi, walifanya hivyo. Kila walichopata, walimtupia.

²²² Vema. Wao walichukua kila nafasi waliyopata kumwangamiza—kumwangamiza Yeye. Wakamswali juu ya

kuzaliwa Kwake. Uzazi Wake ulitiliwa shaka; waliwatupia hilo watu. Wao hawangalifahamu jinsi alivyojaliwa kwa bikira na Yusufu, baba Yake (alidhaniwa kuwa hivyo), seremala; Yeye alizaliwa kabla Yusufu na Mariamu hawajaoana. Waliwatupia hilo watu. Naam, bwana. Ona? Ninasema nini sasa? Wao wanamtia alama nyeusi. Ona?

223 “Mtazame yeye! Alitoka wapi? Mtazame mamaye, si zaidi ya kahaba wa barabarani, alimpata mtoto huyu. Na baada ya huyo mtoto kuzaliwa (alikuwa tayari ana mimba)—huyo mtoto angezaliwa, ndipo Yusufu akamwoa apate kuficha hayo kisha aje huku na baadhi ya . . . Naam, ni kazi ya ibilisi, huwezi kuona hayo? Ni uzazi kama huo!” Waliwatupia watu hilo—kutokusoma katika Biblia, Isaya 9:6, “Bikira atachukua mimba.” Ona, ni nini? Wao waliliacha Neno. Hivyo tu.

224 Wao waliyatupia mamlaka Yake vitu vyeusi. “Mabwana, hamjui ya kwamba sisi ni wanafunzi wa Musa? Hamjui sisi ni watumishi wa Kristo? Hamjui sisi tunayachunguza Maandiko kila siku, nasi hatuna jambo hata moja? Wao walisema Masihi atakuja katika hekalu Lake. Hamna neno hata moja kuhusu Yeye kuja katika hekalu fulani. Yeye yuko wapi? Je, yeye alitoka shule gani? Uliza ndugu ye yote (Methodisti na Batisti na Presbeteria)—mwajua, Mafarisayo, Masadukayo na kadhalika. Yeye anabeba kadi gani ya ushirika? Mamlaka yake angaa ya kuhubiri yako wapi? Yeye hajatiwa mikono bado; hata hana haki ya kuhubiri.”

225 Yeye alisema, “Agizo Langu hutoka kwa Mungu. Kazi Zangu zinadhihirisha Mimi ni nani. (Hiyo ni kweli). Si lazima nipate vyeti vyenu.”

226 Mnaona ninalomaanisha? Walitupa hilo. Mafundisho Yake—naam, walimwita Beelzebuli. Mafundisho Yake, wao hawangalifahamu.

227 Naam Yeye hakubaliani na mafundisho yote ya wazee! Hata hakubaliani na Mafarisayo; hakubaliani na Masadukayo; Yeye anakosa kukubaliana na kundi hilo lote. Basi, yeye anapata wapi mafundisho yake?”

Katika Biblia, bila shaka.

“Vema,” mnasema, “Vema, najuaje ya kwamba hayo ni kweli?”

Mungu huyaunga mkono!

Hivyo ndivyo yule kipofu alivyosema: “Hii ni ajabu iwapo ninyi mko sahihi sana Naye amekosea sana; na huku anaweza kuzitwaa nguvu za Mungu na kuyafumbua macho yangu, na hamjapata kuona hayo yakitendeka hata wa leo! (Hiyo ni ajabu. Salale! napenda kuchagua upande Wake, nanyi je? Bila shaka.) Unasema ya kwamba ninyi ni wanafunzi wa Musa, na mko sahihi

sana Naye amekosea sana; basi hebuni niwaone mkiyatenda mambo anayoyatenda.” Amina!

²²⁸ Hapo ndipo Mafundisho Yake...Wao walimshutumu—madai Yake yote. Walisema, “Hana...Madai yake ni ya uongo ya kuwa Masihi. Angalikuwaje Masihi na asiye kanisani? Angekuwaje Masihi? Sisi hapa mtindi wa Israeli!” Bali huo mtindi umechanguka. Ona? Naam, bwana, na inzi wameuingilia. Kwa hivyo wao—iliwapasa kuuengua.

²²⁹ Kwa hivyo alisema, “Sisi hapa, walio wateule. Sisi—sisi tumeshika yale mapokeo; tumeshika sheria za Musa; tumetenda mambo haya yote na huku chini hivi. Na hapa huyu mtu anakuja na kushutumu madai yetu. Na mbali na hayo, kasisi wetu mtakatifu, baba yetu mtakatifu, aliyetenda *hivi* na aliyetenda *vile* na mambo haya mengine yote, na watu wetu wote walio wakuu—naye anawaita wa ibilisi kisha anajiita Mwana wa Mungu!”

²³⁰ Jamani! Ona, wao walijaribu kutupa vivuli hivyo juu ya Jina la Yesu na kwa Yesu kuyaweka mbele za watu. Kuna mengi sana yangalisemwa hapo, bali inachukua muda mrefu sana. Bali nini? Bali lile Neno na hizo kazi zilimthibitisha Yeye. Amina!

²³¹ Lo, kwa waamini wa kweli, wale waliochaguliwa tangu awali, waliochaguliwa kumwona Yeye na kujua huduma Yake, alikuwa hapo. Hata kama hakufungua kinywa Chake juu ya lo lote, wao walijua alikuwa Hivyo! Haleluia!

²³² Huyo maskini kahaba alienda kule kisimani siku hiyo kuteka ndoo moja ya maji, na mtu mwenye umri wa makamu aliyeketi kule akasema, “Nipe maji ninywe.”

²³³ Yeye akasema, “Naam, si desturi kwenu Wayahudi kumwomba mwanamke Msamaria kitu kama hicho.”

Yeye akasema, “Bali ungalijua ni nani anayekuzungumzia...”

²³⁴ “Sasa,” yeye anawazia, “yeye ni Myahudi kimbelembele sana.” Kasema, “Aa, naona wewe ni Myahudi, na iwapo wewe ni myahudi, bila shaka, wewe ni wa kidini. Nawe unasema tuabudie huko Yerusalemu, lakini baba yetu, Yakobo, alikunywa maji ya kisima hiki na akawanywesha wanyama wake humu, na maji haya yana kina kirefu, na huna kitu cha kutekea; nasi huabudu katika mlima huu...”

²³⁵ Yeye akasema, “Hebu kidogo tu. Nenda kamwite mumeo, mje hapa.”

Yeye akasema, “Hata sina mume.”

²³⁶ Yeye akasema, “Umesema kweli.” Kasema, “Una watano—una watano, na yule unayeishi naye sasa si wako.”

²³⁷ Maskini kahaba huyo—aliychaguliwa tangu awali—naweza kumwona akiweka hicho chombo chini, naye akasema, “Bwana, naona ya kwamba wewe ni nabii.”

238 Ona, ona? Hiyo Mbegu ilikuwa imekaa pale. Kitu tu ilichohitaji ni Maji, nayo Maji tayari yaliisha imwagikia.

239 Yalipowamwagikia hao Mafarisayo, wao walisema, “Ni Beelzebuli.” Haingalizaa kitu, hamna kitu kingalitokea mle isipokuwa magugu.

240 Bali hiyo mbegu iliyochaguliwa tangu asili ilipogusa hayo Maji ya Uzima, yeye alisema, “Bwana, huna budi kuwa nabii. Najua ya kwamba Masihi atakapokuja, Yeye atatufunulia mambo haya yote.”

Yeye akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

241 Alivacha huo mtungi wa maji akaenda zake mjini—alikuwa na jambo la kutangaza. Alisema, “Njoni, mtazame Mtu mbaye ameniambia mambo niliyoyatenda. Je! haimkini huyu ndiye Masihi?” Ona? Yeye alichagua upande wa Yesu. Hiyo ni Kweli.

242 Jambo la ajabu, sivyo? Mafarisayo wote na Masadukayo hawakumjua Yeye na huyu kahaba alimjua. Ona? Kwa nini? Wale waliomwamini na kumpenda na kuona Ishara Zake, wao walijua ya kwamba hiyo ilikuwa Ishara ya Masihi. Hamna kupiga kona; wao walijua hivyo.

243 Mzee Nathanieli alienda kule, labda mbele ya Filipo, kasema, “Sasa, sijui habari hii, Filipo. Nimeona mambo mengi sana yakizuka katika siku hizi za mwisho. Najua kuna mambo mengi sana yanayoendelea.” Bali yeye alienda pale mbele zake na kusema, “Nitamsikiza nisikie anasema nini.”

244 Akaenda zake kule na Yesu kasema, “Tazama, Mwisraeli kweli kweli, hamna hila ndani yake.”

Akasema, “Rabi, ulipataje kunitambua?”

245 Yeye akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwapo chini ya mti nilikuona.”

246 Hiyo... Hayo Maji yakaimwagikia hiyo Mbegu iliyochaguliwa tangu awali. Ilipofanya hivyo, yeye akasema, “Rabi, Wewe u Mwana wa Mungu! Ndiwe Mfalme wa Israeli!”

247 Ilikuwa nini? Hiyo Mbegu ilikuwa mle, tayari, Mungu aliipanda mle nyuma kabla kuwekwa misingi ya dunia, ipate kuleta Nuru wakati uo huo! Haleluya!

248 Huo ndio msimamo wangu papo hapo, Ndugu, hapo ndipo ninapoamini, papo hapo. Nalihubiri nalo linaanguka hapa na pale, na linaenda huku na huko. Haijalishi kamwe, litagusa Mbegu mahali fulani. Na litakapofanya hivyo, itazaa Uhai kama huo, bila shaka. Naam, bwana.

249 Kama huyo mvulana kipofu... Kasema, “Hii ilitendeka kusudi kazi za Mungu zidhihirishwe.” Ona? Yeye alijua yale yatakayotendeka. Bila shaka alijua.

250 Vema. Sasa, wale waliochaguliwa tangu awali, walipoona Ishara Zake za kimaandiko, walijua ya kwamba Neno

lilithibitisha zile kazi—ama zile kazi zilithibitisha Neno, ya kwamba Neno lilikuwa sahihi; hao walichaguliwa tangu awali kuliona, nao walikuwa tayari kuliona, nao wakalipata.

²⁵¹ Kisha wakasema . . . baada ya kuona kwamba hawangalifikia po pote, kwa sababu watu waliochaguliwa tangu awali Uzima wa Milele, wangelipata, na hivyo tu. “Wote alionipa Baba Yangu watanijia. Na wote wajao Kwangu nitawapa Uzima wa Milele na nitawafufua katika siku ya mwisho. Hamna hata mmoja atakayepotea?” Amina! Ni kushikilia hilo tu. Ona? “Si kwa kazi, si kwa matendo, si kwa nguvu, si kwa uweza—kwa Roho Yangu,” asema Mungu. Sasa yale niliyofanya, yale niliyo mimi, ama yale nitakayokuwa; bali yale aliyo Yeye, nami nimo ndani Yake, Na cho chote Yeye alichio, Mimi ni sehemu Yake! Amina! Amina! Mimi nimeokolewa kwa sababu Mimi ni sehemu Yake, Naye ni—Yeye ni Mungu; Mimi ni sehemu Yake, kwa kuwa ni mwanawe. Hiyo ni kweli. Kwa hivyo si yale nimetenda, yale nitakayotenda; ni yale Yeye ametenda. Hayo ndiyo matumaini yangu. Papo hapo.

²⁵² Vema. Kama hivyo wao wakaona ya kwamba hawangalifikia po pote. (Nitaruka Maandiko machache hapa.) Wakaona ya kwamba hawangefikia po pote Naye, kwa hivyo unajua jambo jingine walilolazimika kufanya, kujaribu kumwondoa uwanjani? Wao walienda wakawaambia ndugu Zake na mama Yake, “Mnajua, amechoka sana. Inawapasa kumwondoa mumpeleke pembeni kwa muda mchache.” Hilo kundi la wanafiki. Wao hawaku-. . . Jambo ni kwamba, wao hawakutaka kupata—jambo ambalo hawakutaka kufanya, wao walitaka kumwangamiza. Si eti walidhani alikuwa amechoka sana; wangelitaka afanye kazi hata afe. Bali kila alipoenda kule, miujiza ikaanza kumiminika; Neno la Mungu likaenea. Jamani, si ningalitaka kumsikia akisimama pale siku hiyo kule pwani, na wakati alipomwita Petro na kusema, “Nifuate.” Si ningalitaka kuchukua gogo na kuketi kule, nitupe nyavu zangu na kuacha ndoano yangu, Ndugu Crase, niketi kule na kuegemea kwenye hilo gogo na kumsikiza Yeye akihubiri, alipoingia kwenye huu mtumbwi. Lo, jamani! Si ningalitaka kumsikiza Yeye aliposema ya kwamba, “Njooni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.” Amina! Ningalitaka kumsikia Yeye akisema hayo.

²⁵³ Walijaribu kumfanya mama Yake na wengineo kumwondoa uwanjani. Wao walisema, “Vema, mnajua, yeye—yeye ni mchofu sana. Naamini inawapasa kumwondoa hivyo.” Vyo vyote wangaliweza kumwodosha! Hivyo tu ndivyo walivyotaka. Naam, bwana.

²⁵⁴ Tena wengi waliandamana Naye, kutafuta tu mahali pa kumnasia. Mlijua hivyo? Watu waliomfuata moja kwa moja wakitafuta tu nafasi. Walimpa, siku moja, dinari wakasema, “Rabi (kabla hawajampa dinari)—Rabi, sisi ni Wayahudi.

Tunajua ya kwamba wewe ni mtu mkuu wa Mungu. (Lo, mnafiki huyo! Ona; ona?) Tunajua ya kwamba wewe ni mtu mkuu wa Mungu. Naam, bwana, Rabi! (Wao walikuwa wakiandamana Naye). Ee, habari za asubuhi, Ndugu. Lo, tunashukuru sana umekuja nchini mwetu. Lo, tunashukuru kukuona. Sisi hakika tuko upande wako; meno kwa makucha ya vidole vya miguu, Ndugu. Iwapo utakuwa na ufufuo, huenda tukashirikiana nawe!” Mnaona wanayojaribu kufanya? Kumtega. Ona?

²⁵⁵ Wao walisema, “Basi, tunajua ya kwamba wewe ni mtu mkuu wa Mungu. Wewe huogopi cheo cha mtu ye yote; huogopi kitu ila Mungu. Nasi tunajua ya kwamba wewe ni shujaa. Wewe ni hodari sana kwa ujumbe wako. Tunajua wewe ni nabii mkuu, kwa maana hamna mtu anayeweza kufanya hivyo na kuwa na ujasiri kwa ujumbe wake katika siku kama hizi, isipokuwa alikuwa nabii wa Mungu naye anajua anakosimama. Kwa hivyo sisi tunajua ya kwamba wewe huna upendeleo kamwe. Rabi, wewe ni mtu mkuu. Sisi ni Wayahudi, tuko pamoja nawe, Ndugu; bila shaka! Sasa, Rabi, je! ni halali kumpa Kaisari kodi au siyo?”

²⁵⁶ Lo, hilo kundi la wanafiki! Ona? Roho Mtakatifu alikuwa pamoja Naye; Yeye alikuwa Roho Mtakatifu. Yeye alisema, “Je, mna dinari?”

Kasema, “Ee, ndiyo, ndiyo.” Kasema, “Nina dinari hapa.”

Kasema, “Nipe Mimi.” Kasema, “Je, ni ya nani hii sanamu?”

Kasema, “Ni ya Kaisari.”

Kasema, “Basi, mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na yaliyo ya Mungu mpeni Mungu.”

²⁵⁷ Wakamwekea mtego; wakidai kuwa marafiki Zake. Ilionekana kana kwamba hamna mtu angalimfahamu. Wangesafiri Naye, kidogo, kisha wanaudhika Kwake na kumwondokea. Wao wangesema, “Lo, vema, tulidhania, tulidhania kweli...” Hata wanafunzi walisema, “Tulifikiri hakika huyo alikuwa ndiye atakaye—atakaye-...” Hata Yohana alitumana akamuuliza, “Wewe Ndiye Yule au tumtazamie mwingine?” Ona? Lo, Yeye aliishi maisha ya namna gani (ona?), na akijua hivyo. Bali alikuwa na kusudi moja, kusudi moja—kuifanya kazi ya Mungu.

²⁵⁸ Wengi waliandamana Naye, kusudi tu wapate nafasi ya kumnasia. Sasa, natumaini si kukufuru kama nikisema ni vivyo hivyo siku hizi. Wengi huja na kuifuatilia mikutano kusudi wapate mahali, waone ukimwomba mtu fulani.

²⁵⁹ Hapa si muda mrefu uliopita, dada fulani anayehudhuria kanisa hili, alikuwa katika kanisa lingine, ambapo Mungu alikuwa akifanya kila kitu kitendeka. Naye dada huyo akawaambia dada wengine, kasema, “Mnajua, mtu huyo anayeweza kuomba wagojwa.” Kasema, “Hana budi kuwa na maisha ya u—ushindi sana.” Kisha akasema, “Hana budi,

jamii yake na kila kitu, kuponywa kwa neno lililonenwa, *hivyo*.” [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] Ikawa huyo bibi mwingine alikuwa ametoka Jeffersonville. (Nami; nina hakika hamna mtu apaswaye kujua, ila alivyosema Yesu, “Miongoni mwa watu wenu. . .” Mnajua nchi yenu wenyewe. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo sababu mimi. . . Huenda inakaribia hivi sasa; huenda ikawa ni badiliko la nyakati; mnaona). Naye akasema—akasema, “Mnajua nini?” Kasema, “Hamna hata mmoja wa watoto wake anayeweza kupata homa bila kumpeleka kwa daktari.” Maskini kitu kilichodhiliwa na kudanganyika kama hicho. Ona? Ona, mwanamke ambaye alitaka kulaumu. Kasema, “Watoto wake wanapokuwa wagonjwa, yeye anawapeleka kwa daktari.”

²⁶⁰ Mtu ye yote aliye na hekima atafanya vivyo hivyo. Watu hawawezi kufahamu ya kwamba madawa hutoka kwa Mungu. Naam, ndugu zanguni, kama sivyo, ni ya ibilisi. Bila shaka hutoka huko. Mungu yuko ambako madawa hayawezi kufikia. Bila shaka. Madawa ni Mungu. “Vema,” unasema, “nawajua madaktari wengi sana ambao. . .” Naam, nawajua wahubiri wengi sana ambao wako vivyo hivyo pia! Si mtu ambaye anayashughulikia, ni kile yalivyo. Nawajua watu wengi sana ambao wanashughulikia Neno la Mungu ambao hawaamini katika uponyaji wa Kiungu, hawamwamini Mungu. Sawa. Bali wao wanalishughulikia hata hivyo. Kuna watu wengi walio na madawa na elimu ya upasuaji ambao wanamkana Mungu na kadhalika, bali kuna wengi sana wanaomwamini, pia. Kama inawasaidia watu, ni ya Mungu. Si lazima ni—si lazima nichukue motokaa niende nyumbani usiku wa leo; naweza kutembea kama nilitaka kufanya hivyo, bali Mungu alinitengenezea motokaa, kwa hivyo namshukuru Mungu kwa ajili yake. Mambo haya yote hutoka kwa Mungu, bali yatumie kwa busara; usiwe wazimu nayo. Ona?

²⁶¹ Jambo lile lile. Basi hivyo—ndivyo ilivyo, waona. Kujaribu tu kupata kitu kwa huyo mwongovu mchanga la kuharibu lile jina—lile jina la—la kazi za Mungu. Ona, walitaka kuliharibu. “Kila wakati mtoto akiwa mgonjwa, mmoja wa watoto wake, anawapeleka kwa daktari.” Hakika ningefanya hivyo. Na kama daktari hawezi. . . Nitamsihi Mungu kusaidia kabla ya kuenda huko; ndipo ikiwa daktari hawezi kufanya lo lote la kusaidia, ndipo nitawapeleka kwa mwenye ujuzi zaidi. Hiyo ni kweli. Ndiyo, bwana. Lo, vivyo hivyo leo, wanajaribu kutafuta mtego mahali fulani.

²⁶² Yeye aliwajua, lakini ona, Yeye hakuwakemea kamwe. Yeye aliendelea tu pamoja nao. Yeye hufanya hivyo hata sasa. Huendelea pamoja nao, anawaonyesha neema Yake (hiyo ni kweli) hata ingawa wao wanampinga Yeye. Mbona? Kwa sababu Yeye anawapenda. Na Yeye alienda pamoja nao, lakini daima wako tayari kumwita Yeye kukiwa na haja ya ghafula. Wakati huo wanamtaka Yeye. Hawata-. . .

Watamdhihaki mtu anayepiga makelele. Watamdhihaki mtu anayehubiri uponyanji wa Kiungu, wakisema hawauamini. Ni kwamba tu bado hawajakuwa wagonjwa kutosha. Nimewasikia wengi wa aina hiyo.

²⁶³ Mwanamke alikuwa anakufa, nilipokuwa nikikimbia nikipanda ngazi, nilipokuwa nikihubiri papa hapa, na mwanamme akisimama pale mlangoni akiniita. Mwanamke yule alikuwa ashapita hapa. Aliishi kwa barabara hii huko mbele na alikuwa na ng'ombe pale. Naye akasema, "Kama ng'ombe wangu angepokea namna ya dini ambayo Billy ako nayo, ningemuua yule ng'ombe." Kabla ya saa moja haijaisha akawa mgonjwa na kupelekwa hospitalini—mwanamke kijana mrembo. Nami nikaharakisha kuenda huko. Mmewe alikuwa Mkatoliki na walitumana niitwe. Yuafa, na akaenda...na macho yake yakaanza kuvimba, akasema, "Mwite; mwite; mwite; mwite, haraka, haraka."

²⁶⁴ Na ndugu ya huyo mwanamke akakimbia humu na kusimama pale mlangoni na kungoja na kungoja, na kuendelea kumpungia mkono. Mahali hapa pamejaa watu, na baada ya muda mfupi mtu fulani akaja na kuweka tangazo hapa mezani; lilisema—sema, mtu anakufa hospitalini. Na ninaamini ni Ndugu Grim Snelling...Nilisema, "Chukua mahali pangu nikiisha enda." Naye alikuwa akisimama apate kuongoza uimbaji; alikuwa hata hajaitwa na ku kuhubiri wakati huo. Akapanda kuja kuongoza uimbaji, nami nikatoka na kuingia katika gari langu na kuenda huko haraka, na nilipokuwa tu nikipanda vile vipandio akavuta punzi yake ya mwisho. Na bila shaka, matumbo na figo ni kila kitu kikakoma. Na nikakimbia mle ndani, na walikuwa wamefunika uso wake, na mvuke ukipanda pale namna hiyo; na yule mkunga mzee akisimama pale, akasema, "Ndugu Branham, alipaza sauti katika pumzi yake ya mwisho akikuita." Akijaribu kutubu, lakini alikuwa amechelewa zaidi wakati huo. Waona? Unaweza kutenda dhambi zaidi mara moja zaidi na kuvuka mpaka, wajua. Naye alikuwa kama ana-...katika uso wake...

²⁶⁵ Alikuwa na nywele nyekundu—mwanamke mrembo mno. Naye—nywele zake zilizonyolewa zilikuwa zimetoka matita-matita; macho makubwa mekundu yalijitokeza na kufungwa nusu tu. Na madoa katika uso wake yalikuwa katika njia fulani, katika mvuto mkuu, mpaka yakaonekana kama vilima katika uso wake, na mdomo wake ulikuwa wazi. Na nikaenda pale na kumtazama na pale mmewe alisimama na kusema, "Billy, hivi ndivyo ilivyokuwa." Kasema, "Mimi ni Mkatoliki. Ninataka useme sala kwa ajili yake, kwa sababu ameenda purgatorio."

Nami nikasema, "Ati nini?"

²⁶⁶ Kasema, "Sema sala kwa ajili yake." Kasema, "Yeye ameenda purgatorio. Alipita karibu na kanisa lako yapata saa

mbili zilizopita na kusema kama ngombe wetu atapokea dini kama yako, angemuua yule ng'ombe." Ona? Kasema, "Sema sala kwa ajili yake."

²⁶⁷ Nikasema, "Amechelewa zaidi, alipaswa kuitakasa nafsi yake hapa, sio mpaka afike mahali pengine." Ona? Hiyo ni sawa. Lo, ndiyo. Lakini daima twamhitaji Yeye wakati wa huzuni. Watu, nimewasikia wakisema, "Mimi simuamini Mungu." Mwache ajiumize vibaya sana mara moja; ona Yule atakayemwita kwanza.

²⁶⁸ Hata wanafunzi Wake, wakati mmoja walipokuwa katika dhoruba, hata ingawa walipomwona Yeye, walimwogopa Yeye kidogo. Hawakujua hasa ilikuwa ni nini. Walisema, "Hiyo ni roho, na wakalia kwa sauti kuu." Hata hivyo matumaini yote ya kuokolewa yalipokwisha, kwa hivyo wakamkaribisha Yeye ndani. Ndiyo, daima wao wana...uwe mwenye kushuku kidogo au la. Wakati matumaini yote hayapo, wanapenda kumkaribisha Yeye ndani. Ndiyo. Walimpokea Yeye ndani, kwa sababu walikuwa na haja na Yeye. Hiyo ni kweli.

²⁶⁹ Unajua, mara nyingi nimeshangaa, wakati mwingine pengine hiyo ndiyo sababu zile dhoruba zinakuja. Je, umeshawahi kufikiria jambo hilo? Yeye aliketi pale juu na kuwatazama mpaka walipokuwa na haja Naye, na ndipo Yeye akaja hadharani. Basi taweza kuona haja yetu ya kuwa Naye sasa. Twaona kuwa dhoruba inakuja, wandugu. Hebu na tuwe upande Wake usiku huu, tuwe upande wa Neno Lake. Ni—nitamalizia hapa.

²⁷⁰ Hebu na tuwe upande Wake. Hebuni ninyi na mimi, wandugu, tuungana pamoja na Yeye usiku huu. Ile dhoruba inakuja. Na usingoje mpaka ule mtumbwi mdogo umezama. Na tumpokee Yeye katika mtumbwi wetu mdogo sasa. Ungeangalia huko na kusema, "Siwezi kuelewa mambo haya yote, Ndugu Branham."

²⁷¹ Tuangalie kama tunasema lo lote ila lile ambalo liko katika Neno. Ona kama kuna lo lote ila lile Yeye aliahidi kufanya lingeonekana kama ndoto kwako wakati mwingine. Unafikiri, "Ole wangu, siwezi kuelewa hilo." Lakini siku yaja ambapo uzima wako huu utaondoka. Haitaonekana baya sana kwako wakati huo. Wakati unajua, wewe mwenyewe, yakubidi umgeukie yule Mungu aliyekuumba, utataka kumwingiza Yeye ndani wakati huo. Na tukamwingize Yeye ndani sasa, kabla ya dhoruba kuwa mbaya zaidi ya ilivyo sasa.

²⁷² Ninataka Yeye—a—ndani ya roho yangu. Ninamtaka Yeye sana katika maisha yangu mpaka utu wangu uloweke kabisa, ili nia yangu, mawazo yangu, cho chote nilicho mimi, kimetawaliwa na kuongozwa na Kristo Yesu. Ninataka nipotee sana kwa—kwa nafsi yangu hata yote nitakayojua na kuona ni Yesu Kristo. Na kama...Ningependa kuja mbele yenu wote...Kama

Mungu wa Mbinguni atawaruhusu muwe na haya yote ambayo nimewaambia habari zake, nijapo miongoni mwenu, ningetaka kumuona Kristo naye amesulubiwa. Ni—ninataka kujua ule utukufu na sifa za dhamani za Mungu; nikae miongoni mwenu na kumsikia mhudumu mmoja akisimama na kutoa sifa kwa Mungu kwa ajili ya yale ameona yakifanyika kanisani mwake; na mwingine yale aliyoona yakifanyika kanisani mwake; na mwingine yale aliyoona yakifanyika kanisani mwake. Hayo hasa ndiyo waliyofanya.

²⁷³ Na walipokuja pamoja na kukutana katika ushirika katika Matendo 4, walipewa habari za yale Mungu alifanya *hapa*, na yale Mungu alifanya *hapa*. Na Petro na Yohana walikuwa wamepigwa na—na—na kufanywa waahidi kwamba ikiwa wata—yale ambayo wangepigwa kama wangepigwa tena katika Jina la Yesu. Nao wakakusanyika pamoja na watu wao, na wote wakaomba kwa nia moja, na kuomba katika mapenzi ya Mungu na kunukuu Maandiko, “Mbona mataifa wamefanya ghasia, na makabila wametafakari ubatili.” Na walipoomba, Roho Mtakatifu alitikisa mahali walipokusanyika pamoja. Hiyo ndiyo namna ya mkutano tunaohitaji. Hiyo ndiyo yatupasa tuwe nayo, wandugu.

²⁷⁴ Hebu na tukakingwe na Neno la Mungu, na Roho wa Mungu, na Nguvu za Mungu, na hebu Nuru yetu ing’ae sasa, tuwe kama Stefano.

²⁷⁵ Alisimama pale, mtu mmoja mbele ya baraza la Wayahudi la pengine watu nusu milioni wakisimama pale, kila mmoja wao akimlenga kidole cha kumshtaki usoni mwake. Wakati yule mtu mdogo alipotembea pale nje, yasema aling’aa kama malaika. Simaanishi pengine Nuru usoni mwake hivyo; malaika hana haja kuwa na Nuru juu yake. Bali malaika ni mwanamume—malaika ni mjumbe, na mjumbe anayejua yale anayosema. Katembea pale nje na kusema, “Ndugu zangu na baba zangu, baba zetu katika Mesopotamia...”—vile walivyotolewa huko... na Ibrahimu na wengineo, na mpaka mahali fulani. Halafu akafika mahali pa kuharibu na kusema, “Enyi wenye shingo gumu, msitahiriwa mioyo wala masikio, mbona siku zote mnampinga Roho Mtakatifu? Kama baba zenu walivyofanya, na ninyi ni vivyo. Alijuwa hasa kile alichokisimamia. Hiyo ndiyo sababu alikuwa aking’ara. Hakuogopa hata kidogo; alimjua Yule aliyemwamini.

²⁷⁶ Hata wakati mauti yalipobisha kwenye mlango wa moyo wa Mtakatifu Paulo na akasema, “Namjua Yeye niliyemwamini, na kusadiki ya kwamba aweza kukilinda kile nilichokiweka amana kwake hata siku ile.” Amina!

²⁷⁷ Bwana awabariki nyinyi, wandugu. Ninasikitika kuwakawisha hapa mpaka saa tano kasoro dakika ishirini na tano. Ninajua hii si kawaida kwenu. Ninasikitika kufanya

hivyo, lakini mmekuwa wazuri sana usiku huu; hakuna hata mmoja wenu aliyeondoka. Mmeketi na kupeana usikivu wenu wote; na ninatumaini kuwa katika hotuba yangu ndogo, iliyovunjikavunjika, yenye woga, kwamba Mungu, yule Roho Mtakatifu, mahali fulani amemwaga mbegu ndogo ndani ya mioyo yenu, kwamba uweza wa Mungu utaigusa na kuihuisha, kama yule mwanamke pale kisimani, na wengine walioteuliwa Uzima wa Milele. Mungu ambariki.

²⁷⁸ Ndugu Neville, utawaruhusu waende, au unataka ku...? Una...Tu...Mnampenda Yeye? [Makutano wanajibu, “Amina”—Mh.] Mtamtumikia Yeye? [Makutano wanajibu, “Amina.”—Mh.] Amina!

Mnampenda Yeye? Amina
 Mtamtumikia Yeye? Amina
 Mtamwamini Yeye? Amina, Amina, Amina.
 Tunataka tuuimbe. Amina
 Amina, Amina, Amina, Amina.
 Biblia ni kweli, Amina
 Ninaiamini Amina.
 Ni Neno La Mungu. Amina, Amina, Amina.

Hebu na tusimame.

Amina, Amina, Amina, Amina, Amina.
 Bwana, tunakupenda Wewe,
 Amina, Amina. Amina, Amina, Amina.
 Tunaamini Wewe unakuja. Amina
 Tuko tayari kukutana na Wewe. Amina.
 Njoo, Bwana Yesu. Amina, Amina, Amina.
 Twaomba Mungu aturuhusu kuwa wazuri
 tuwezavyo nyakati zote kumtumikia Yeye.
 Amina, Amina, Amina, Amina, Amina.
 Ninatumaini kuwa yeye atawabariki ninyi,
 na kuwahifadhi ninyi, na kuwaweka ninyi,
 na kutuangalia sisi, na kuwatia moto hata
 kuingia katika Ufalme Wake kufanya kazi
 kuu, na kunisaidia mimi uwanjani mpaka
 tukutane tena.
 Amina, Amina, Amina, Amina, Amina.
 Nitawaombea ninyi, nanyi mtaniombea mimi?
 Amina, Amina, Amina, Amina, Amina.

²⁷⁹ Baba wetu, tumekusanyika usiku huu katika Jina Bora la Bwana Yesu. Jina hilo penzi na tamu ambalo sote twalipenda na kuliabudu. Ninafikiri jinsi makundi ya watu katika miaka iliyopita (kwa miaka thelathini au zaidi tumekusanyika katika jengo hili ndogo na zee), jinsi tungekaa kuzunguka jiko miguu yetu ikiwa karibu kuganda kwa baridi; na kuketi pale na miguu yetu juu ya jiko na kuzungumza kuhusu Bwana Yesu. Ninafikiri juu ya miguu kadhaa ya dhamani iliyotembea juu

ya hii nchi, waliokaa na hiyo miguu juu pale. Ninafikiria mzee Ndugu Seward, Ndugu Sparks, Ndugu George De Ark, wapenzi wengine wa dhamani walioketi na miguu yao juu ya jiko, wameenda kukutana na Bwana wao usiku huu, wakipumzika kule ng'ambo kaburini, walingoja ule mwito mkuu wa kuenda juu. Walivipiga vita, wailinda imani, wameumaliza mwendo, na sasa wanaingoja taji ya haki ambayo Bwana, Hakim wa Haki, atawapa siku hiyo.

²⁸⁰ Baba Mungu, tuliomba tulipolizidua kanisa hili dogo hapa pembeni na kusema, “Bwana Yesu, na lisimame na watu wawe ndani yake wakati Wewe utakapopasua anga na kuja katika kule kuondoka kwa siri kwa kanisa”. Mungu, ninaomba kwamba nafsi waliokuja hapa madhabahuni, na waliokutumikia Wewe, ile Mbegu ya Injili ambayo imepandwa huko na huko, huko na kule, na huko na kule hapa kwa miaka thelathini, kwamba twaamini wengi wa watu hawa wa dhamani watakuwepo pale siku hiyo, kwa sababu ya juhudi hizi dhaifu ambazo tumezitoa kuleta lile Neno kwa ule Uzima uliochaguliwa tangu asili. Tunakushukuru Wewe kwa ajili hiyo na kutumaini, Mungu, usiku huu kwamba kusiwe na ye yote aliye hapa sasa ambaye hatakuwepo siku hiyo, akiwa amefunikwa na ile Damu, ametia nanga katika Yesu. Tujalie hili, Baba. Tunamtumaini Yeye.

²⁸¹ Sasa, tutakutana hapa tena Jumapili asubuhi, wengi wetu. Na tunaomba, Mungu, kwamba Wewe utakutana nasi na kutumegea Mkate ulio Hai. Mungu, tungependa kumkumbuka Ndugu Ruddle na mahali pake pale juu, ambapo wale wanaosafiri pamoja naye... Kuwa pamoja na yule kijana wa dhamani, Bwana, ninaomba ninapomwona akikua, waone hawa vijana. Ninasikia kama hawa ni ma Timotheo wangu. Ninaomba, Baba, kwamba utambariki Ndugu Ruddle katika huduma yake. Mbariki Ndugu “Junie” Jackson. Enhee Mungu, tunaomba kwamba baraka Zako ziwe juu yake na juu ya Ndugu Crase, juu ya Ndugu Snelling, juu ya ndugu huyu mwingine pale anayechukua mahali pake, na Ndugu Beeler, na Ndugu—wandugu hawa wote hapa, Bwana, na Ndugu Neville, na kila mmoja wetu, Bwana. Tunaomba tu kwamba baraka Zako zitakuwa juu yetu, kuwa neema Yako ndiyo tu tunayohitaji, Bwana, tuweze kuendelea. Na tusije tukasahau yale masimulizi madogo ya usiku huu: hata ingawa yule mwanamke mdogo akisimama pale bila kujua mwisho utakuwaje; lakini Yesu alihitaji kutushughulikia, naye alikuwa akimshughulikia. Ndiyo, akamtawadha miguu Yake, jambo lililopuuzwa ambalo hata waliodai kuwa watumishi Wake walishindwa kufanya, na walikuwa wakijaribu kumdhihaki, lakini yule mwanamke akamtumikia Yeye, bila kutarajia zawadi; na hapana zawadi kuu zaidi ambayo ingetolewa.

²⁸² Mungu, hebu na tufanye hivyo, kuendelea tu mbele na kufanya kazi ya Mungu. Na yote tunayotumania sana

kufanya, Bwana, ni kusikia katika siku ile, “Vema, mtumwa Wangu mwema na mwanifu. Ingia katika furaha ya Bwana uliyoandaliwa kabla ya kuwekwa misingi dunia.” Mungu atujalie kufanya hivyo na kuweka ushirika mmoja na mwingine; na hebu Roho Mtakatifu awe pamoja nasi, na kutuongoza, na kutuelekeza katika yote tufanyayo, na kutupa maisha marefu, pengine kama yawezekana, tuone kule kuja kwa Bwana Yesu. Tunaomba hayo katika Jina Lake. Amina.

Kibarikiwe kifungo
Kitufungiacho mioyo,
Ushirika wetu na fikira zetu
Ni kama ule wa mbingu.
Tutawanyikapo mbali,
Hiyo yatufadhaisha;
Lakini tungali pamoja rohoni
Hata tutakutanika.

²⁸³ Biblia ilisema waliimba wimbo na kutoka nje. Mungu awabariki ninyi sasa hata niwaone tena Jumapili asubuhi, Bwana akipenda. Kwaherini.



Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Pili
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume Two)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org